4 APRILI, 2023

# BUNGE LA TANZANIA

___________

# MAJADILIANO YA BUNGE

___________

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 4 Aprili, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI ZILIIMBWA**

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

## HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na: -

**SPIKA:** Hati za kuwasilisha mezani, Waziri Mkuu, kwa niaba yake Mheshimiwa Patrobass Katambi, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):**

Randama za Makadirio ya Bajeti, Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na taasisi zake kwa mwaka 2023/2024 kama ifuatavyo:-

(i) Fungu 25 - Ofisi ya Waziri Mkuu;
(ii) Fungu 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa;
(iii) Fungu 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu;
(iv) Fungu 65 - Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi,Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu;
(v) Fungu 15 - Tume ya Usuluhishi na Uamuzi;
(vi) Fungu 42 - Ofisi ya Bunge;
(vii) Fungu 61 - Tume ya Taifa ya Uchaguzi;
(viii) Fungu 91 - Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Matumizi ya Dawa za Kulevya;
(ix) Fungu 92 - Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali na tutaanza na Ofisi ya Rais -TAMISEMI. Mheshimiwa Mhandisi Ezra John Chiwelesa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi sasa aulize swali lake.

Na. 1

**Kukamilisha ujenzi Vituo Vya Afya – Biharamulo**

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Vituo vya Afya vya Rugaragata, Kalenge na Nyabuozi – Biharamulo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais – TAMISEMI Mheshimiwa Dkt. Dugange majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa, Mbunge wa Jimbo la Biharamulo Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vituo vya afya vya Rugaragata, Kalenge na Nyabuozi ni miongoni mwa vituo vya muda mrefu na miundombinu yake inahitaji maboresho kulingana na mahitaji ya sasa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2023/2024 Serikali itatenga bajeti ya shilingi bilioni 8.75 kwa ajili ya ujenzi, upanuzi na ukamilishaji wa vituo vya afya 20 katika Halmashauri, ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Biharamuro iliyotengewa shilingi milioni 500 kwa ajili ya upanuzi wa vituo vya afya viwili kati ya vitatu vyenye mahitaji.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kutenga bajeti kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa vituo vya afya chakavu ni endelevu. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Ezra Chiwelesa, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Naomba nifanye masahihisho kidogo, kituo kinaitwa

Rukalagata, Kata ya Biharamulo Mjini, kingine ni Kalenge Kata ya Kalenge na kingine ni Nyabusozi Kata ya Nyabusozi.

Mheshimiwa Spika, tarehe 9 Novemba 2022 nilisimama hapa ndani nikiongelea Kituo cha Rukalagata kwamba hakina jengo la upasuaji na bahati nzuri nikajibiwa na Waziri wa Fedha kwamba nilete maombi maalum na wao watanitengea pesa kwa sababu hospitali ya Biharamulo Mjini imejengwa lakini iko nje ya Mji kwa hiyo watu wa Biharamulo Mjini hawapati huduma. Barua yetu ilitoka Tarehe 14 siku tatu zilizofuata…

**SPIKA:** Swali lako Mheshimiwa Ezra ni lipi?

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Swali la kwanza je, hii barua ilishapokelewa na imefika kwa Waziri wa Fedha? Je, *status* ikoje, kama haijafika naomba niikabidhi hii barua.

Pili, napenda nishukuru kwa sababu nimeambiwa vituo viwili vitafanyiwa kazi. Ni hayo tu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa, Mbunge wa Jimbo la Biharamulo Magharibi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nimepokea marekebisho, pili kwa kuwa barua iliwasilishwa na Halmashauri ya Biharamulo kwenda Wizara ya Fedha, Ofisi ya Rais -TAMISEMI tutafanya mawasiliano ya karibu na Wizara ya Fedha baada ya maswali hapa na tuone kama barua imeshafika na tuone

hatua za utekelezaji ili ahadi ya Serikali ya kuleta fedha hiyo iweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, pili, hivi vituo vya afya viwili ambavyo vimetengewa shilingi milioni 500 ni vile kati ya vituo vya afya vitatu ambavyo Halmashauri mtaona kipaumbele ni vipi vianze ili tuanze kukarabati na kuanza kutoa huduma hizo. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Rose Busiga, swali la nyongeza.

**MHE. ROSE V. BUSIGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nami naomba niulize swali la nyongeza.

Je, katika hizo fedha shilingi bilioni 8.75 Kituo cha Afya cha Nkhomola kitakuwa ni miongoni mwa vituo vya kupatiwa hizo pesa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Rose, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, fedha hizi ambazo zimetengwa shilingi 8,750,000,000 zitakwenda kuainisha vituo vya afya 20 vyenye uchakavu wa hali ya juu zaidi. Kwa sababu sina orodha hapa naomba kwa ridhaa yako baada ya kipindi hiki nitaangalia na kuona kama kituo hicho ambacho amekitaja Mheshimiwa kipo kwenye orodha hiyo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, swali la nyongeza.

**MHE. JULIANA D SHONZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru; wananchi wa Kata ya Sanga katika Wilaya ya Mbozi wamejenga boma la kituo cha afya; je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa kituo hicho? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Juliana Shonza, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kata ya Sanga ambayo wananchi wamejenga boma kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya ni sehemu ya Kata nyingi kote nchini ambazo wananchi wamejenga, Serikali imeweka mpango mkakati, kwanza kukamilisha vituo vya afya ambavyo ujenzi wake umeanza lakini baada ya kukamilisha vituo hivyo tutakwenda awamu ya pili ya kuainisha maboma na kuanza kuyakamilisha na wakati huo tunatoa kipaumbele pia katika jengo hili la kituo cha afya cha Sanga, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi; kwanza ninaipongeza Serikali imejenga vituo vya afya vingi sana ndani ya Halmashauri ya Tanganyika, tuna tatizo la ukosefu wa vitendea kazi kwenye vituo vya afya pamoja na watumishi.

Je, ni lini Serikali itapeleka vitendea kazi na watumishi kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Vijijini, Kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba vituo vingi vya afya vimejengwa lakini katika mwaka wa fedha huu Serikali imetenga zaidi ya bilioni 193 kwa ajili ya kupeleka vifaatiba katika vituo vilivyojengwa. Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi kwamba kwa kiasi kikubwa vituo vyetu vimeanza kupokea fedha na vifaatiba kwa ajili ya kutoa huduma.

Mheshimiwa Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba zoezi hili litaendelea katika vituo vya afya vya Halmashauri ya Tanganyika. Ahsante sana

**SPIKA:** Mheshimiwa Jerry Silaa, swali la nyongeza.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana; Zahanati ya Mongo la Ndege imejengwa kwa kipindi kirefu tokea nikiwa Diwani wa Ukonga.

Je, Serikali haioni sasa kutokana na ongezeko la wakazi kwenye mtaa wa Mongo la Ndege na maeneo jirani ya Jimbo la Segerea ni wakati sasa wa kupandishwa hadhi na kuwa kituo cha afya? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jerry Silaa, Mbunge wa Jimbo la Ukonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Zahanati ya Mongo la Ndege inahitaji kupanuliwa na kupandishwa hadhi kuwa kituo cha afya, kwa awamu hii tunaendelea kwanza na ukamilishaji wa zahanati na vituo vya afya ambavyo kazi ya ujenzi imeanza.

Mheshimiwa Spika, ninatoa wito kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilala kuona uwezekano wa kutenga fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya kuanza kupandisha hadhi kituo hiki cha afya cha Mongo la Ndege. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Kata ya Uyui ambayo ndiyo kata kubwa kuliko kata zote katika Jimbo la Tabora Mjini haina kabisa kituo cha afya na tulikwishaomba muda mrefu ili iweze kupata kituo cha afya.

Je, ni lini Serikali itatupatia kituo cha afya katika Kata hiyo ya Uyui?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kata zote ambazo zina vigezo vya kujengewa vituo vya afya zitaingia kwa awamu baada ya

kukamilisha vituo vya afya ambavyo vinaendelea kujengwa. Serikali imekwishatoa maelekezo kwa Halmashauri zenye mapato ya ndani yanayozidi bilioni tano, kuanza ujenzi wa vituo hivyo kwa kutumia ile asilimia 60 na asilimia 70 ya mapato ya ndani. Kwa hiyo, nitoe maelekezo pia kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Tabora kuanza kutenga fedha kwa awamu, wakati Serikali pia inatafuta fedha kwa ajili ya kupandisha hadhi lakini pia kujenga kituo cha afya katika kata hii, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa David Mathayo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Kata ya Makanya katika Jimbo la Same Magharibi kimechakaa sana na ni cha zamani sana.

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha katika Halmashauri ya Wilaya ya Same ili kukarabati kituo cha afya cha Makanya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa David Mathayo Mbunge wa Same Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Makanya ambacho amekitaja Mheshimiwa Mbunge ni sehemu ya vituo ambavyo ni chakavu na Serikali inaendelea kuweka mpango mkakati wa kuvikarabati. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Mbunge aamini kwamba Serikali imetambua

hilo, tunaweka mpango endelevu wa kukarabati na kituo hiki kitapewa kipaumbele. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vedastus Manyinyi swali la nyongeza.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Bweri ni kati ya vituo vya afya vya kwanza cha kwanza kujengwa pale katika Manispaa ya Musoma lakini hakikukamilika na kimechakaa sana pamoja na kituo cha Makoko.

Je, ni lini sasa Serikali itatoa fedha ili tuweze kuvimalizia vituo hivyo viwili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vituo vya afya ambavyo Mheshimiwa Mbunge amaevitaja, kituo cha Bweri na Makoko ni sehemu ya vituo ambavyo Serikali inaweka utaratibu mahsusi kwa ajili ya kutenga fedha na kuvikarabati, vile ambavyo miundombinu haijakamilika vinatengewa fedha kwa ajili ya ukarabati na kujenga majengo hayo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako. Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya Mbunge wa Manyoni Mashariki sasa aulize swali lake.

Na. 2

**Barabara ya kutoka Kintinku-Makanda kuhamishiwa *TANROADS***

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA** aliuliza: -

Je, ni lini barabara ya kutoka Kintinku hadi Makanda inayounganisha Mkoa wa Singida na Dodoma itahamishiwa *TANROADS*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais – TAMISEMI Mheshimiwa Deo Ndejembi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Jimbo la Manyoni Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007, kifungu cha 11 na Kanuni za Usimamizi wa Barabara ya mwaka 2009 kifungu 43(1) na (2) na kifungu 44(1) kupitia Tangazo la Serikali Na. 21 ya tarehe 23 Januari 2009, zimeainisha vigezo na utaratibu wa kuhamisha barabara ili iwe chini ya *TANROADS* ambapo barabara inaweza kupandishwa au kuteremshwa toka daraja moja kwenda daraja lingine.

Mheshimiwa Spika, suala la kupandisha hadhi barabara ni la kisheria na kuzingatia vigezo. Ili barabara iweze kupanda kutoka daraja la barabara ya Wilaya kwenda daraja la barabara ya Mkoa (kusimamiwa na *TANROADS)* inatakiwa barabara hiyo ijadiliwe kwenye Kikao cha Bodi ya Barabara

ya Mkoa husika na ikionekana inakidhi vigezo, Bodi hiyo kupitia kwa Mwenyekiti itamshauri Waziri mwenye dhamana na barabara kuwa barabara husika imekidhi vigezo na hivyo ipandishwe daraja na kuwa chini ya *TANROADS*.

Mheshimiwa Spika, hivyo, nashauri utaratibu wa kuhamisha barabara kwenda *TANROADS* uzingatiwe ikiwemo kwa hii ya Kintinku - Makanda kwenda *TANROADS*.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, najua mnajadili mambo ya msingi sana na ya muhimu sana kwa ajili ya Taifa hili, lakini katika hiyo mijadala punguzeni sauti kidogo ili majibu ya Waziri yasikike na ili maswali ya nyongeza yanayoulizwa yatokane na majibu ya Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, punguzeni sauti wakati mkijadili hayo mambo muhimu kabisa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya, swali la nyonyeza.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili ya nyongeza: Je, ni lini ujenzi wa Daraja la Ntumbi ambalo linaunganisha barabara ya Ntumbi - Nangongo utaanza kufanya kazi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili: Nini mpango wa Serikali wa kuweka taa za barabarani katika Mji wa Manyoni ili kuweza kuboresha ulinzi na usalama wa Mji wa Manyoni?

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa daraja la Ntumbi, tayari bajeti ilikuwa imeshatengwa shilingi milioni 496 na tayari usanifu ulikuwa umeshafanyika na sasa wapo katika hatua za kutangaza ili daraja hili liweze kujengwa na wananchi wa Mheshimiwa Chaya pale na Watanzania wale wa Manyoni waweze kupata huduma ya barabara hiyo kupitika.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili kuhusu taa za barabarani, katika mwaka huu wa fedha tayari bajeti ilikuwa imetengwa kwa taa 15. Kwenye hili pia nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kulifuatilia sana. Tayari katika bajeti ya mwaka wa fedha unaofuata zimetengwa taa 28 pale Manyoni Mjini ambapo tutaenda kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Phillipo Mulugo, swali la nyongeza.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru nami kupata kupata nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Waziri vikao vya *RCC* Mkoa wa Songwe vimekuwa vikipitisha barabara ya kutoka Kapalala kwenda Buha kilometa 36 kila mwaka toka nimeingia Ubunge, lakini hatujawahi kupata majibu ya kwamba barabara hiyo imepandishwa hadhi. Kila wakati tunakaa tunapeleka, tukaa tunapeleka, na leo mmesema ndiyo vikao halali vinavyopitisha. Lini barabara hiyo itakuwa ya hadhi ya *TANROADS?*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Phillipo Mulugo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi, suala hili likishapitishwa kisheria kwenye vikao husika linakwenda kwa Waziri mwenye dhamana ya barabara ambaye ni Waziri wa Ujenzi. Sasa sisi kwa pamoja kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi tutalifuatilia na Mheshimiwa Mbunge tutaona wapi ambapo japo hili limekwama na tutampatia majibu, lakini dhamana yake ipo kwa Waziri wa Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa ujenzi wa kilomita moja ya lami Makao Makuu ya Wilaya ya Nyang'hwale pale Kalumwa, mkandarasi aliingia kwa kasi kubwa na akaweka vifusi na akashindilia; na baada ya hapo hajaweka lami; na leo zaidi ya miezi mitatu haonekani *site;* tatizo ni nini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hussein Amar, Mbunge wa Nyang'hwale kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tutalifuatilia jambo hili, na tutawasiliana na Meneja wa *TARURA* wa Mkoa wa Geita na vilevile wa Wilaya ya Nyang'hwale kujua ni kwa nini mkandarasi huyu amekwama kuendelea na kazi hii? Vilevile nitakutana na Mheshimiwa Mbunge tuweze kulitafutia

majawabu leo hii hii hapa tukiwa katika viwanja vya Bunge. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Je, ni lini barabara ya kuanzia Mzumbe kibaoni kwenda mpaka Lubungo mpaka Kibambila ambayo ni Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero, mpaka Kimamba, Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa itajengwa na kupitika kwa mwaka mzima kwa kuunganisha wilaya zote mbili? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ishengoma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tutalifuatilia suala hili kwa kuona barabara hii kama imetengewa bajeti katika mwaka huu wa fedha tunaokwenda. Nafahamu Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Angellah Kairuki amekaa na Waheshimiwa Wabunge wa Mikoa yote na kuangalia vipaumbele katika barabara, afya na elimu. Hivyo, tutaangalia kama barabara hii na yenyewe imo ili tuone ni namna gani ambavyo tunaweza tukawafikia wananchi hawa wa kwa Mheshimiwa Ishengoma.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Kassinge, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona kwa nafasi ya swali la nyongeza. Barabara ya kutoka Hoteli tatu mpaka Pande na hatimaye Limalyao katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa imeshafanyiwa

mapendekezo ya kupandishwa hadhi ili iwe ya *TANROADS* na vikao husika. Lini Serikali itapandisha hadhi barabara hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ally Kassinge, Mbunge wa Kilwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotoa majibu ya awali kwa Mheshimiwa Mulugo na Mheshimiwa Chaya, ili kupandisha hadhi barabara hizi, baada ya mchakato wote kuwa umeshapitiwa, sasa ni mamlaka ya Waziri mwenye dhamana ya barabara ni Waziri wa Ujenzi. Sasa wakati tunafuatilia suala la Mheshimiwa Mulugo tutahakikisha na hili la Mheshimiwa Kassinge nalo tunaliangalia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa barabara ya kutoka Kolandoto kwenda Kishapu ni barabara muhimu sana kwa uchumi wa Kishapu: Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mnzava, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali hii ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeweka kipaumbele sana katika kuhakikisha barabara zetu zinapitika wakati wote ikiwemo barabara hii ya Kolandoto kwenda Kishapu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tutaliangalia suala hili na kuona ni namna gani barabara hii nayo itaweza kuwekewa fedha na kuweza kutengenezwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Shally Josepha Raymond.

Na. 3

**Sheria kuruhusu Halmashauri kukopesha *SACCOS* za Vijana na Wanawake**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND K.n.y. MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali italeta Sheria Bungeni kuruhusu Halmashauri kuzikopesha *SACCOS* za vijana na wanawake?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tena, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mikopo ya asilimia 10 inatolewa kwa mujibu wa kifungu cha 37A cha Sheria ya Fedha za Serikali za

Mitaa Sura ya 290. Kifungu hicho kimeeleza kwamba Halmashauri zote zinapaswa kutenga asilimia 10 ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya mikopo isiyo na riba kwa vikundi vilivyosajiliwa vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Spika, mikopo ya *SACCOS* huendeshwa kwa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha (Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo) ya mwaka 2019 ambapo mikopo hiyo hutolewa kwa wanachama wa *SACCOS* kwa riba. Hivyo, mapendekezo ya kurekebisha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura ya 290 ili kuzikopesha *SACCOS* kutaondoa kusudio la kutoa mikopo isiyo na riba kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa mikopo hiyo kutokuwa na riba ni kivutio kikubwa sana kwa wale ambao hawana uwezo; na wakati huo huo wanawake wana vikoba: Je, Serikali inaonaje sasa kama wale wa vikoba watapatiwa mikopo hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shally Raymond Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sheria ya mikopo ya asilimia kumi imeeleza kwamba wajasiriamali wanawake, vijana na watu wenye ulemavu wanaweza kukopeshwa wakijiunga kwenye vikundi vyao na mkopo huo hauna riba. Kwa hiyo, kama wanawake walio kwenye vikoba ni sehemu ya kikundi cha

wajasiriamali bila kujali kwamba wapo kwenye vikoba au la, wataweza kukopeshwa fedha hizo kwa utaratibu huo na kufanya shughuli zao ili kujiletea maendeleo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima Mdee, swali la nyongeza.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, asilimia 10 tuliipitisha kwa mabadiliko ya Sheria ya mwaka 2019, lakini Taarifa za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusiana na asilimia 10 ya mwaka 2021 zilipotea shilingi bilioni 47.5; za mwaka 2021/2022 iliyotoka juzi, zimepotea shilingi bilioni 88.

Mheshimiwa Spika, swali langu kwa Waziri; kwa kuwa Wakurugenzi ambao ndio *accounting officers* wamepewa majukumu ya kusimamia hizi fedha kuhakikisha zinawafikia watu sahihi, lakini Wakurugenzi hawafanyi hivyo, matokeo yake fedha nyingi zinapotea: Ni lini Serikali inapanga kuchukua hatua kali za kisheria dhidi ya *accounting officers* huko kwenye Halmashauri zetu wanaoshindwa kutekeleza majukumu yao?

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli moja ya changamoto kubwa katika mikopo ya asilimia 10 ni kasi ya maejesho kwa vikundi vilivyokopeshwa. Serikali imetambua changamoto na ndiyo maana katika miaka mitatu mfululizo, kasi ya urejeshaji imetoka asilimia 62 mwaka 2018/2019 mpaka asilimia karibu 80 mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto hiyo Serikali imeendelea kuchukua hatua kwa *accounting officers,* kwa maana ya Wakurugenzi katika Halmashauri zetu ambao walithibitika kutosimamia ipasavyo marejesho ya mikopo ya asilimia kumi. Zoezi la kuchukua hatua kwa *accounting officers* ni endelevu. Kila mara Serikali itakapotambua kwamba kuna Mkurugenzi hajatimiza wajibu wake na fedha hazijarejeshwa, lazima atachukuliwa hatua kwa mujibu wa taratibu za utumishi na kwa mujibu wa taratibu za kisheria, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Genzabuke, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza nampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uamuzi wake kwamba asilimia zilizokuwa zikikopeshwa kwenye Halmashauri zipitie benki:-

Mheshimiwa Spika, sasa kwa kuwa wanawake na vijana watakuwa wanakopeshwa kupitia benki: Je, ni kwa nini sasa Serikali isiamue vikundi ambavyo ni vya wanawake na vijana vilivyounda *SACCOS* navyo viunganishwe katika kukopeshwa kupitia benki? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika,...

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, amesimama Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Angellah Kairuki.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Genzabuke na pia nimpongeze

sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Dugange kwa majibu mazuri yenye umakini mkubwa sana; na niwashukuru kwa maswali yote yaliyoulizwa na Waheshimiwa Wabunge wote; Mheshimiwa Shally Raymond pamoja na Mheshimiwa Halima Mdee.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tayari Mheshimiwa Rais ameshaelekeza kwamba tutakuwa na mfumo mpya wa utoaji wa mikopo hii ya asilimia 10, napenda tu kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba tumeshaanza kuandaa utaratibu na pindi utakapokuwa tayari, tutawajulisha na tutaweza kujua katika benki tutakuwa kwa mfumo wa aina gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutaendelea kupokea maoni yoyote yatakayoboresha namna gani katika benki pia mfumo huu uweze kutumika na tunawashukuru. Kikubwa tunawaomba, kwa zile ambazo tayari zilishatolewa na zilishakopeshwa, tulishaanza kuingia mikataba na walionufaika na mikopo hii na ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba fedha zote ambazo zilitolewa tangu mikopo hii kuanza kutolewa zinarudishwa na ndiyo moja ya fedha hizo hizo pia tutakazozitumia katika kupeleka katika benki zetu na kuzikopesha kwa ajili ya utaratibu mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niendelee kuwasisitiza na kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa wanaingia Mabaraza ya Madiwani, kuhakikisha kwamba fedha zote zilizokopeshwa nyuma zinarudi, na pia bado tunaendelea kupokea ushauri kwamba ni namna gani tunaweza tukatekeleza vyema katika huo mfumo mpya utakaotolewa katika benki zetu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Juma Usonge Hamad, Mbunge wa Chaani, sasa aulize swali lake.

Na. 4

**Kukamilisha Miradi ya Mazingira na Tabianchi Zanzibar**

**MHE. JUMA USONGE HAMAD** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha Miradi ya muda mrefu ya Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi inayotekelezwa Zanzibar?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mheshimiwa Hamza Hamza, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Usonge Hamad Juma, Mbunge wa Chaani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaratibu miradi miwili kwa Upande wa Zanzibar. Mradi mmoja wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa Kutumia Mifumo Ikolojia Vijijini *(EBARR)* unaotekelezwa kwenye Wilaya ya Kaskazini A, Unguja; na Mradi wa Kurejesha Ardhi Iliyoharibika na

Kuongeza Usalama wa Chakula katika Maeneo Kame Nchini *(LDFS)* unaotekelezwa katika Wilaya ya Micheweni, Pemba.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha miradi hii inakamilika kwa wakati, tayari Serikali imechukua hatua za kiutendaji kuwataka waratibu na washughulikiaji wa miradi hii kitaifa kuhakikisha miradi inakamilika kikamilifu na kwa ubora. Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais inaendelea kuwasiliana na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar ili kusimamamia utekelezaji wa miradi hiyo kwa upande wa Zanzibar ili miradi hii ikamilike kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Usonge Hamad Juma, swali la nyongeza.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa vile Mheshimiwa Waziri amekiri kabisa kwamba katika miradi hiyo kuna changamoto ya ucheleweshwaji; naiomba sana Serikali, kama itaridhia.

Kwa nini kwa mwaka wa fedha huu isikamilishe miradi hii kwa kutumia fedha za ndani badala ya kusubiria fedha za wahisani, ambapo hadi leo hii ni muda wa miaka mitano miradi ile haijakamilika?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kufuatana nami kwenda kuiona miradi hiyo inayotelelezwa kwenye wilaya mbili ilivyosimama na bado hatma ya kukamilika miradi hiyo haijulikani? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba

kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Juma Usonge Hamad, Mbunge wa Chaani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, miradi hii ambayo inatekelezwa Zanzibar, takribani ukiangalia miradi yote; ile ya *EBARR* na hii ya *LDFS* ni miradi ambayo kwanza fedha zake zipo, lakini ni miradi ambayo ukiiangalia muda wake wa kukamilika bado yaani haujafika, kwa sababu miradi hii ukamilikaji wake ni mpaka 2024.

Mheshimiwa Spika, nimwambie tu Mheshimiwa Usonge kwamba pamoja na kwamba miradi hii ina fedha za wahisani, lakini pia kuna fedha ambazo zinatoka kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, zinakwenda kukamilisha miradi hii. Kwa hiyo, nimwambie Mheshimiwa asiwe na hofu.

Mheshimiwa Spika, suala la kufatana naye kwenda kukagua miradi hii, nimwambie tu kwamba niko tayari, kama ambavyo nimeshaanza mara ya kwanza, tutakwenda naye kukagua miradi hii na kuona ukamilifu wake na namna ambavyo inanufaisha wananchi. Nakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe.

Na. 5

**Utafiti juu ya kuyeyuka kwa theluji ya Mlima Kilimanjaro**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya utafiti wa sababu za kuyeyuka kwa theluji ya Mlima Kilimanjaro na kukauka kwa vyanzo vya maji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Hai, Mkoa wa Kilimanjaro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Tanzania inayo mipango na mikakati ya kuendelea kufanya utafiti wa sababu za kuyeyuka kwa theluji ya Mlima Kilimanjaro na kukauka kwa vyanzo vya maji. Kupitia Taasisi mbalimbali za ndani ya nchini, zikiwemo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, na Chuo Kikuu cha Nelson Mandela, vinaendelea kufanya tafiti kuhusu suala hili. Baadhi ya sababu zilizobainika kuchangia hali hiyo ni pamoja na kuongezeka kwa wastani wa joto duniani, shughuli za binadamu zinazoendelea, ukataji wa miti na uchomaji misitu ovyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuhimiza uongozi na wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro kuongeza jitihada za kutunza mazingira ya mlima huo kwa kudhibiti uchomaji moto ovyo na kuongeza jitihada za kuhifadhi mazingira na kupanda miti.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, hali ya Mlima wa Kilimanjaro ni mbaya sana. Swali la kwanza kwa kuwa Serikali inakusanya fedha nyingi kutokana

na Mlima Kilimanjaro, ni lini Serikali itatenga fungu maalum kwa ajili ya utafiti huo aliousema na pia *operation* maalum ya kupanda miti katika Jimbo la Hai?

Mheshimiwa Spika, la pili, mara kadhaa nimekuwa nikiomba Fedha za *CSR* na sijapata majibu humu ndani. Je, Serikali haioni ipo haja ya Wizara hizi mbili ya Muungano na Mazingira pamoja na Utalii kukaa kwa pamoja na kutengeneza mkakati kwa kuhakikisha tunaondoa tatizo la mabadiliko ya tabia nchi katika Mlima Kilimanjaro? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongenza ya Mheshimiwa Saasisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimwambie tu Mheshimiwa kwamba tupo tayari kutenga hilo fungu lakini n kiukweli miti mingi hapa katikati ilikufa kutokana na hali ya joto, kutokana na miti kuchomwa hovyo na kukatwa hovyo. Ofisi ya Makamu Wa Rais, Muungano na Mazingira, tayari tumeshakaa kwa kushirikiana na halmashauri na taasisi za kifedha zikiwemo *CRDB*, *NMB* na kwa kushirikiana na *TFS* tayari tumeshaanza huo mchakato wa upandaji miti.

Mheshimiwa Spika, nimwambie pia tuna kampeni yetu ya kusoma na mti ambapo tunashirikisha wanafunzi wa awali, msingi, sekondari, vyuo na vyuo vikuu, tunawahamasisha wapande miti. Jitihada zote tulizozichukua zitafika Kilimanjaro zitafika Hai na miti itapandwa na mazingira tutayatunza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili nimwambie kwamba tumekuwa mara kadhaa tumekuwa na Wizara ya Maliasili kwa sababu tunaamini kwamba wao ndio wenye miti kupitia

*TFS* ya kuweza kupanda. Sisi tupo tayari kupanda miti Kilimanjaro. Lakini tumwambie tu Mheshimiwa Mbunge yeye sasa aanze kuchukuwa juhudi ya kuanzisha hiyo Kampeni, halafu sisi kwa kushirikiana na wadau wengine tutakuja tuje tuifanye Kilimanjaro iwe ya kijani na kuhakikisha kwamba miti inapandwa na mazingira yanatunzwa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, swali la nyongeza.

**MHE. ANNE K. MALECELA**: Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata hii nafasi. Matukio ya kudhoofisha Mlima Kilimanjaro yanatupunguzia *pride* ya sisi Watanzania kwa sababu Mlima Kilimanjaro ni *pride* kwa nchi yetu. Hivi Serikali hamuoni kwamba kuna umuhimu wa kuweka uzito mkubwa kuyaangalia hayo matukio yanayotokea mara kwa mara ili kuurudisha mlima wetu katika hali ambayo sio ulivyo sasa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Waziri amesimama, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Selemani Jaffo, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA**: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze Naibu Waziri kwa ufafanuzi mzuri na majibu mazuri ya awali lakini Mlima Kilimanjaro ni kweli ni fahari yetu sisi Watanzania na kwa mfano mwaka jana tulipokuwa na kesi ya uwakaji wa moto Mlima Kilimanjaro, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ilifanya kazi kubwa sana na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa sababu Mlima ule upo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulienda pale kama timu na kupanga mikakati mbalimbali chini ya *KINAPA*. Kwa hiyo, ni kweli jambo hili la Uwakaji wa moto kwa sababu tuliunda timu kwa ajili ya kufanya utafiti nini sababu ya kuwaka moto, je ni hujuma ama ni nini? Lakini jambo hilo nadhani Serikali tunaendelea vizuri na nikuhakikishie Mama Anne Kilango Malecela, sisi dhamira yetu ya dhati ni kuhakikisha Mlima Kilimanjaro unaendelea ku-*survive* vizuri zaidi. Lakini niwaombe sana wanachi wa Mkoa Kilimanjaro wakati tunapanda karibuni mita 3,700 pale tumegundua kuna watu wanafanya shughuli mle ya ukati wa miti na uchomaji yaani ni changamoto kubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwaombe wananchi wote kwamba suala la kuutunza Mlima Kilimanjaro ni jukumu la kwetu sote sisi Watanzania kwa sababu linatuletea uchumi wa hali ya juu kubwa kwa hiyo tuna kila sababu kuulinda fahari hii sote kwa pamoja kwa ajili ya nchi yetu Tanzania. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI**: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa. Wananchi wanaoishi katika vijiji vinavyozunguka Mlima Kilimanjaro hushindwa kuripoti changamoto za kiusalama kule mlimani kama kukata miti na moto kutokana na uhaba au uhafifu wa mawasiliano. Je, Serikali ina mpango gani kusaidia kuboresha mawasiliano katika vijiji vinavyozunguka Mlima Kilimanjaro?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja

la nyongeza la Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hii changamoto kweli tumeiona, *sometimes* unafika wakati kunatokezea majanga ya moto na mambo mengine, wananchi wanashindwa kuweza kutoa taarifa na sisi kama Serikali tukachukua hatua kwa wakati. Nimuambie tu Mheshimiwa kwamba hili jambo tunalichukua na tunakwenda kulifanyia kazi ili matukio yakitokea tuhakikishe kwamba sisi yanatuletea taarifa mapema na tunayachukulia hatua zinazofaa kwa mujibu yaani kwa wakati unaohusika.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphance Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHANCE N. BUTONDO**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Wilaya ya Kishapu ni moja kati ya Wilaya ambazo zipo katika mkakati na mapambano ama kampeni za mabadiliko ya tabia nchi katika Kata ya Alagana pamoja na Kata ya Kiloleli, ipo miradi iliyotekelezwa hasa ya mabwawa ya mifugo ambayo kimsingi miradi hiyo imetekezwa chini ya kiwango.

Je, Mheshimiwa Waziri upo tayari kuambatana na mimi kwenda Jimboni kwangu kujenga miradi hiyo na kushauri namna bora amna namna gani ya kuweza kuirudia na kuitekeleza upya? *(Makofi)*

**SPIKA**: Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumshukuru kaka yangu Mbunge wa Kishapu, nadhani swali lake lilikuwa

linaendena na lile swali la kwanza la EBA, kwa sababu tuna Mradi wa *EBA* umetekelezwa katika halmashauri tano ikiwepo na Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu sasa kwa vile swali hili lilikuwa linaenda katika upande ule wa Saasisha swali la Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, kiufupi niseme ni kwamba Mheshimiwa Mbunge nitaambatana na wewe tuende tukafanye kuangalia kama kuna mapungufu ya aina yoyote kuweza kuyafanyia kazi kama Serikali, ni jukumu letu kulifanya. Lakini binafsi naomba niwashukuru hawa Wabunge wa Kishapu, Wabunge wa Nzega, Wabunge wa Mkalama, Wabunge wa Mvomero na Mpwapwa katika mradi huo wameutendea haki sana kusimamia vizuri katika maeneo mbali mbali tumepata mafanikio makubwa. Kwa hiyo, Mbunge *this is my commitment* kwamba tutaenda pamoja kutembelea. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, Mbunge wa Tunduru Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na. 6

**Mradi wa *REA II* – Tunduru Kaskazini**

**MHE. HASSAN Z. KUNGU** aliuliza:-

Je, ni lini Mradi wa *REA II* utakamilika katika Vijiji 23 vilivyobaki vya Jimbo la Tunduru Kaskazini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Stephen Lujwahuka, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, Mbunge wa Tunduru Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Pili ulitekelezwa na Mkandarasi *LTL* ambapo jumla ya vijiji 36 vya Wilaya ya Tunduru vilipatiwa umeme na mradi ulikamilika Mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* inatekeleza Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili katika Jimbo la Tunduru Kaskazini ambapo unatekelezwa na Mkandarasi *M/S JV Guangdong Jianneng Electric Power Engineering Co. Ltd. and White City International Contractors Ltd.* unalenga kupeleka umeme katika vijiji 23.

Mheshimiwa Spika, Mkandarasi yupo katika maeneo mbalimbali ya mradi akiendelea na kazi za ujenzi wa miundombinu na kuunganisha wateja. Mradi unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Desemba, 2023.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, niishukuru na kuipongeze Serikali kwamba imeongeza kilometa mbili za usambazaji wa umeme katika kila kijiji na kuifanya kilometa tatu badala ya kilometa moja; je, ni lini sasa Serikali itaanza utekelezaji huo wa kujazilizia kilometa mbili ili kila kijiji kipate kilometa tatu za usambazaji wa umeme? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika,swali la pili, kwa kuwa mradi huu wa *REA* vijijini ni mradi wa umeme vijijini; je, ni lini sasa Serikali itapeleka umeme vitongojini? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kungu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwenye swali la kwanza ni kweli Serikali ya Awamu ya Sita iliongeza kilometa mbili kwa kila kijiji ambacho kipo katika Mradi wa *REA III Round Two* ambao unaoendelea kutekelezwa. Kazi iliyofanyika ni kupitia maeneo yale ya vitongoji na kuyabaini ili hizo kilometa mbili zionekane wapi zipelekwe.

Mheshimiwa Spika, ninavyozungumza majadiliano na wakandarasi yanaendelea na tunaamini kuanzia mwanzoni mwa wiki inayokuja hiyo mikataba ya *adendum* mikataba ya nyongeza ya kupeleka umeme kwenye hizo kilometa mbili itasainiwa na hivyo tunatarajia mwanzoni mwa mwezi wa tano wakandarasi wataingia *site* kuendelea sasa na hiyo kazi ya kupeleka umeme katika hizo kilometa mbili za nyongeza ambazo zinatakiwa ziongezwe.

Mheshimiwa Spika, kwenye swali la pili kwamba ni lini umeme utapelekwa vitongojini. Nipende kusema hata sasa umeme unapelekwa kwenye vitongoji, Miradi ya rea inapeleka umeme vijijini ambapo vijiji vinaenda kwenye vitongoji, lakini upo mradi maalum wa *densification 2B* ambao unaendelea katika vijiji karibu 1,600 na wakandarasi tayari wameripoti *site* na wanapeleka umeme katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa zaidi Serikali ipo katika taratibu za mwisho za kutafuta fedha kupeleka umeme kwenye vitongoji karibu 6101 ambavyo bado havijapata umeme na inahitajika takribani shililingi trilioni 6.5 ambayo tunaamini tutaipata kwa mbinu ambazo tayari tumepeleka maombi yetu Serikalini na mchakato wa kutafuta pesa hiyo unaendelea. Hivyo katika miaka minne mitano tunatarijia kuwa tumemaliza vitongoji vyote ambavyo havina umeme na huo ndio mpango wa Awamu ya Sita.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nawaona mmesimama wengi, maswali mnauliza marefu kwa hiyo muda unaniishia kwa sababu kila mmoja anataka kutoa historia ya jambo lake, historia ya kijiji kwa hiyo muda unaniishia. Kwa hivyo tuuwiane radhi kwa sura hiyo, kwa sababu mnaomaliza muda ni ninyi. Mheshimiwa Abubakari Asenga. Wale watakaoitwa usipoenda kwenye swali nitakukata.

Mheshimiwa Abubakari Asenga, swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, Je, ni lini Wizara itatekeleza maelekezo ya Mhesimiwa Waziri January Makamba kwa kurejesha bei ya kuunganisha umeme kwa Tarafa ya Ifakara mathalani maeneo yote yale ambayo yana asili ya vijiji 27000 kwa mfano Katinduka B na C

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi. Halafu Mheshimiwa Naibu Waziri ukiwa unajibu mtazame Spika kwa sababu ndiyo unayezungumza naye. Ahsante sana.

Majibu kwa kifupi ili iwe unajua nikiwasha hapa unajua muda umekwisha, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kubaini maeneo ya kupelekea umeme kwa gharama ndogo ulifanyika lakini haukuwa makini vya kutosha kwa hiyo tumewaelekeza wenzetu wa *TANESCO* warudie zoezi hilo tena kwa kuwa -*consult* Waheshimiwa Wabunge wote ili tupate maeneo hayo na kuyafanyia kazi sahihi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Timotheo Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha unaharakisha na kukamilisha kupelekwa kwa umeme kwenye vijiji vya Wilaya ya Korogwe kwa sababu mkandarasi wake anasuasua sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mnzava, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli mkandarasi anayepeleka umeme kwenye Wilaya ya Korogwe pamoja na nyingine mbili anazembea sana na tumekubaliana achukuliwe hatua na itakapofika katikati ya mwezi huu kama atakuwa hajafikia yale makubaliano tuliyofikia basi hatua stahiki zitachukuliwa ikiwemo pamoja na kuvunja mkataba wake ambao ameshindwa kuutekeleza kwa wakati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona; je, ni lini Serikali itapeleka huduma ya umeme wa *REA* katika Kijiji cha Tilawandu ambacho kilisahaulika katika awamu zilizopita za utekelezaji wa umeme wa *REA*? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu naomba kujibu naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Francis Ndulane, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vijiji vyote ambavyo vilikuwa havina umeme vipo katika mradi wa *REA* Awamu ya III Mzunguko wa Pili na kwa sasa tuna takribani vijiji 2,600 tu ambavyo vimebaki havina umeme kabla ya Disemba vitakua vyote vimepata umeme.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mkundi, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mhesimiwa Spika, nashukuru, ni, lini Serikali itakamilisha usambazaji umeme kwenye visiwa vidogo vilivyoko nje ya Gridi ya Taifa Jimboni Ukerewe? Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa ya Mheshimiwa Joseph Mkundi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tumeshatangaza zabuni tayari kwa ajili ya wapelekaji wa umeme katika maeneo ambayo hayajafikiwa na Gridi na kinachofanyika sasa ni mchakato wa kubaini bei na uhalisia wa huduma yao ili tuweze kufikisha umeme katika maeneo ambayo Gridi ya Taifa haijafika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nicodemas Maganga, swali la nyongeza. *(Makofi)*

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Vijiji 34 Mbogwe havijawekewa umeme kabisa, ni lini vitawekewa umeme, vijiji vya Mbogwe ambavyo havijapata umeme toka dunia iumbwe? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maganga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vijiji vyote ambavyo havina umeme viko katika mradi wa *REA III Round Two* na tunaendelea kusimamia na wakandarasi kuhakikisha kabla ya Disemba hii kukamilika basi vijiji vyote vimepata umeme kwa mujibu wa mikataba yetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY A. J. JUMBE:** Mheshimiwa Spika, *ETBICO* ni Kampuni ambayo inasambaza umeme Mkoani Mbeya imekua ikidanganya kwamba imewasha umeme wakati inangurumisha *transformer,* je hii ni sahihi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, sijasikia vizuri, samahani naomba arudie.

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa unaambiwa hujasikika. Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe, swali la nyongeza. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. ALLY A. J. JUMBE:** Mheshimiwa Spika, *ETBICO* wanaenda vijijini, kwa mfano Kijiji cha Bukunelo, Kijiji cha Ikama wanasema wamewasha umeme na taarifa Serikalini ni kwamba imewasha umeme, wakati huo wamewasha *transformer* zinaunguruma na umeme wenyewe kwa wananchi haujafika, je hiyo ni sahihi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Ally Jumbe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuwasha umeme kwa mwananchi ni kumwashia katika nyumba yake na eneo lake analohitaji umeme. Kwa hiyo, kama wanasema wamewasha kwenye *transformer* hiyo sio sawa na tutalifuatilia kuhakikisha kwamba umeme unawafikia wananchi kwa sababu ndio wanaouhitaji. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Nicholaus Ngassa, swali la nyongeza.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, Kata ya Isakamariwa, Kilinginira, Kilungu, Mwamwashiga na Mtungulu mkandarasi kaweka nguzo, je, ni lini atakamilisha kuweka waya wawashe umeme? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali mawili la nyongeza la Mheshimiwa Ngassa, kwamba kabla ya Disemba hii kuisha vijiji vyote na kata zote na maeneo ambayo yapo katika Mradi wa *REA III Round Two* yatakuwa yamewashiwa umeme.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, ni mara ya tatu au zaidi nauliza hili swali nilitaka kufahamu ni lini Mkoa wa Kagera utaunganishwa kwenye Gridi ya Taifa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tayari fidia imeshafanyika katika njia ya kutoka Benako kuja Kyaka kwa ajili ya kupitisha umeme utakaotoka Nyakanazi na Rusumo kuja katika Mkoa wa Kagera na Serikali kupitia *BADEA* imepata fedha za utekelezaji wa mradi huo, kwa hiyo, siku sio nyingi mambo yataanza kufanyika katika eneo la *site*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Janeth Maurice Massuburi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 7

**Kudhibiti madereva wasiotii Sheria za Usalama Barabarani**

**MHE. JANETH M. MASSABURI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatunga Sheria kali za kudhibiti madereva wasiofuata sheria za usalama barabarani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Maurice Massaburi**,** Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usalama Barabarani, sura 168 ya mwaka 1973 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2002 na kanuni zake, inayotumika Tanzania Bara, na Sheria ya Usafiri Barabarani, Sura ya 7 ya mwaka 2003 na kanuni zake, inayotumika Zanzibar, zinatoa adhabu kwa wale wanaokiuka Sheria ya Usalama Barabarani. Serikali inaendelea kuboresha Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usalama barabarani ambao tayari ulishasomwa kwa mara ya kwanza hapa Bungeni ili kuzingatia mabadiliko yaliyotokea na mahitaji ya sasa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Janeth Massuburi, swali la nyongeza.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa moja ya sababu inayosababisha ajali nyingi hapa nchini ni wembamba wa barabara zetu, Je, Serikali haioni haja ya kuruhusu magari makubwa ya mizigo kutembea nyakati za usiku? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je, ni umri upi unaoruhusiwa kutoa leseni kwa madereva wa magari makubwa? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Janeth Massaburi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja, kuhusu wembamba wa barabara; ni kweli taarifa za utafiti zinaonesha wembamba wa barabara ni moja ya sababu inayosababisha ajali na hili linafanyiwa kazi na wenzetu wa Uchukuzi na Usafirishaji, ambao ni Wajumbe wa Baraza la Taifa la Usalama barabarani na ndio maana mtaona wakati mwingine tunapanua barabara kule upande wa Mbeya na maeneo mengine inavyoonekana imekuwa changamoto.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, magari ya mizigo yatembee usiku; nadhani sio suluhisho la kudumu kwa sababu tunataka nchi yetu ichangamke kwenye biashara, hatuwezi kuacha kusafirisha wakati wote tukisubiri wakati wa usiku tu.

Mheshimiwa Spika, tunachotakiwa kufanya ni kuimarisha usimamizi wa sheria za usalama barabarani na kuboresha miundombinu ya barabara ili kuwe na usalama wakati wote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umri unaofaa kwa mtu kupewa leseni ya kuendesha magari ya mizigo ni mtu mzima, na kwa Tanzania mtu mzima baada ya miaka 18 amefanya mafunzo na amefuzu kwa vigezo vyote anaweza akapewa leseni ya kuendesha magari.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mjini Dar es Salaam kumejengwa barabara…

**SPIKA:** Unaongeaje Mheshimiwa, atakusikia kweli? Ama leo swaumu imeanza asubuhi? *(Kicheko)*

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, katika Mji wetu wa Dar es Salaam kumejengwa barabara ya njia nane, lakini madereva wengi hawajui matumizi ya barabara ile.

Je, ni lini Serikali itaendesha mafunzo ya kutumia ile barabara kwa sababu unakuta guta limekaa kwenye *highway* badala ya kukaa kwenye barabara ya upande wa kushoto. Je, Serikali ni lini itatoa mafunzo rasmi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zuberi Kuchauka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama Wabunge wanafuatilia na wananchi kwa ujumla kazi inayofanywa na chombo chetu cha usalama barabarani *(traffic police)* wanatoa elimu kupitia vyombo vya habari kuhusu usafiri kwenye kipindi cha UBA, usafiri na uraia Tanzania. Pale hutoa mafunzo mbalimbali juu ya namna barabara zile zinavyotakiwa kutumika. Kwa gari yoyote inayokwenda mwendo mdogo au inaelekea kusimama inatakiwa itembee kushoto zaidi na gari ambayo inakwenda haisimami kwenye vituo vya karibu inatakiwa ipite kule kule ambako wanaita *highway*. Kwa hiyo elimu hii itaendelea kutolewa ili kuwe na matumizi sahihi ya barabara hizi, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wakati ukimjibu Mheshimiwa Massaburi maswali yake ya nyongeza kuhusu magari kutembea usiku nilikuwa najiuliza ya abiria yanaruhusiwa kutembea usiku?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, yanaruhusiwa mpaka saa sita usiku na kwenye maeneo ambayo yana changamoto za usalama na

barabara zake ni mbovu tumezuia kabisa, hasa kwa maeneo kama Tabora kwenda Katavi ni *risk* kutembeza magari usiku; na ndiyo maana tunawashauri wahakikishe wanapanga ratiba zao ili wapite maeneo hayo kukiwa bado mchana.

**SPIKA:** Nafikiri hili jambo nilishawahi kulisemea mahali pengine. Ni muhimu Serikali ilitazame kwa ujumla wake. Tunazuia magari saa sita kwa sababu ipi? Kwa sababu madereva ni wale wale wanaotuendesha sisi na wanaoendesha yale magari mengine, madereva wanapitia masomo yale yale.

Kama kuna mahali kuna mapungufu tuyafanyie kazi hayo mapungufu; lakini kuzuia abiria halafu anakaa hapo halafu gari inaondoka baada ya saa nne, labda saa kumi usiku au saa 11 ndipo zinaondoka. Sasa sijui tunakuwa tumezuia nini; hasa katika kipindi hiki ambacho Serikali inafanya juhudi kubwa sana ya kuboresha miundombinu ya barabara. Sasa zile barabara tunazitengenza kwa ajili ya kazi gani? kwa sababu yule abiria angekuwa na gari binafsi maana yake angeweza kutembea huo usiku, lakini kwa kuwa hana anatumia basi kwa hivyo inabidi asubiri. Sasa yeye tunamchelewesha wa kazi gani? kwa hiyo mlitazame Serikali maeneo ambayo miundombinu ya barabara haina shida kabisa na usalama uko vizuri, waruhusuni watu watembee usiku. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, tumepokea ushauri, tutaufanyia kazi na kutoa maelekezo ipasavyo.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Bahati Khamis Kombo, Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi sasa aulize swali lake.

Na. 8

**Ukarabati wa Jengo la Kituo cha Polisi Kengeja**

**MHE. BAHATI KHAMIS KOMBO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itafanya ukarabati wa Jengo la Kituo cha Polisi Kengeja?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bahati Khamis Kombo, Mbunge toka Baraza la Wawakilishi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Jengo la kituo cha Polisi Kengeja, Mkoa wa Kusini Pemba ni chakavu na halifai kwa matumizi ya kutoa huduma za Kipolisi. Makadirio ya gharama za kujenga kituo kipya cha Polisi daraja C yamefanyika ambapo kiasi cha shilingi 292,544,139 zitahitajika. Fedha hizo zitaombwa kutoka mfuko wa tuzo na tozo ili ujenzi wake uanze katika mwaka wa fedha 2023/2024.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bahati Khamis Kombo, swali la nyongeza.

**MHE. BAHATI KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kuwa kituo hiki hakiwezi kutoa huduma; je, ni mpango gani wa dharura ambao wameuweka ili kulinusuru lile jengo pamoja na wafanyakazi walioko pale?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bahati Khamis Kombo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mpango wa dharura ambao tumekuwa nao ni kutumia Kituo cha Polisi cha jirani cha Mtambile iwapo wataona jengo lile linazidi kuwa hatarishi kwa watumiaji.

Mheshimiwa Spika, lakini tumebaini kuwa kituo hiki kiko umbali wa kilometa nane kutoka pale mkoani; kwa hiyo tutakachofanya ni kuharakisha kujenga kituo hiki mara baada ya bajeti yetu kupitishwa mwezi Julai ili huduma zianze kutolewa kwenye kituo ambacho ni salama zaidi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Minza Mjika swali la nyongeza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, je, ni lini Serikali itakarabati majengo ya Kituo cha Polisi Maswa ili yaweze kuendana na hadhi ya Wilaya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kutoka Mkoa wa Simiyu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Maswa kweli ni cha siku nyingi na kimechakaa. Maelekezo yetu kwa *IGP* na wasaidizi wake kule mikoani wafanye tathmini ya kiwango cha uchakavu na kubaini gharama zinazohitajika ni kiasi gani ili kiweze kupangiwa matengenezo kadiri tutakavyopata fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, swali la nyongeza.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri alikuja Jimboni kwangu Mchinga na kuona hali halisi ya Kituo kile cha Mchinga na Gereza la Kingurungundwa; je, ni lini vituo vile vitajengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, tunakiri kwamba Kituo cha Mchinga na Gereza la Kingurungungwa kama alivyotaja ni chakavu sana na tayari tumeingiza kwenye mpango wa bajeti wa mawaka 2023/2024. Mara tutakavyoidhinisha bajeti, fedha zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa Kituo cha Mchinga na ujenzi *actually* wa kituo kipya na ukarabati wa Gereza la Kingurungundwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omar Omar swali la nyongeza.

**MHE. OMAR ALI OMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana; nami nataka niulize swali moja la nyongeza.

Mkoa wa Kaskazini Pemba kituo cha polisi kiko katika hali mbaya; je, Serikali inampango gani wa kukitengeneza kituo hicho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Omar Omar kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli nilitembelea Pemba na nilibaini kituo kile kweli ni chakavu. Kinachotia faraja ni kwamba mkoa umeshabaini eneo la kujenga kituo kipya cha ngazi ya mkoa. Katika bajeti yetu ya mwaka ujao ni mpango wa Serikali kuanza ujenzi wa Kituo kipya cha Polisi cha Mkoa wa Kaskazini Pemba.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Flatei Gregory Massay Mbunge wa Mbulu Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 9

**Ujenzi wa Barabara ya Haydom – Katesh**

**MHE. FLATEI G. MASSAY** aliuliza: -

Je, ni lini barabara ya Haydom kwenda Mogitu - Katesh itajengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandisi Msongwe Kasekenya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa

barabara hii, Wizara kupitia *TANROADS* tayari imeingia mkataba na mhandisi mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, kufanya tathmini ya athari za kimazingira na uandaaji wa nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara ya Haydom – Katesh yenye urefu wa kilometa 70. Kazi ya Usanifu imeanza mwezi Februari, 2023 na inategemewa kukamilika mwezi Februari, 2024. Baada ya usanifu kukamilika na gharama za ujenzi kujulikana, Serikali itatafuta fedha za kuanza ujenzi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa barabara hii ina vipande vingi; je, kipande hiki cha Labay kwenda Hydom na cha Dongobesh kwenda Dareda mnakijenga lini?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa kipande hiki cha Mbulu kuja Garbabi mmeshamuweka mkandarasi pale na yuko *site* na hamjamlipa *advance payment* na hajengi tena barabara;

Je, ni lini mnamlipa *advance payment* ili ajenge barabara au mpaka turuke tena?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kipande cha Mbulu- Garbabi mkandarasi yuko *site,* nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hajatoka *site* yupo; na mudo siyo mrefu fedha aliyokuwa anaidai, kwa sababu ilikuwa ni sanifu na jenga, italipwa muda siyo mrefu na kwa hiyo tunaamini kwamba kasi itazidi.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Dareda – Dongobesh ipo kwenye hatua za manunuzi na sasa tuko kwenye hatua ya majadiliano na mkandarasi. Ahsante

**SPIKA:** Mheshimiwa Leah Komanya swali la nyongeza. Mheshimiwa Leah Komanya, Waziri wa Fedha amesimama. Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri. Nilitaka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na wala asiruke sarakasi tena, fedha ile Wizara ya Ujenzi walishaleta maombi yale na tunakamilisha maandalizi tutatoa ile fedha ili mkandarasi asikwame. Na tumeongea na wenzetu wa Wizara ya Ujenzi tutapata majumuisho hata maeneo mengine ambayo yalikuwa na uhitaji wa aina hiyo ili tuweze kukamilisha na kazi zisikwame.

**SPIKA:** Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya swali la nyongeza.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru; je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami kilometa 25 katika maingilio ya Daraja la Sibiti ili kunusuru mmomonyoko kwa kuwa barabara iko juu ya mbuga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Leah Komanya, Mbunge wa Meatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Daraja la Sibiti linatakiwa kujengwa *approach roads,* yaani barabara za maingilio kilometa 25. Taratibu za kumpata mkandarasi ambaye atajenga zinaendelea. Hata hivyo bado katika hii barabara ndiyo barabara ambayo mpango wa *EPC+F* barabara ndefu pia itapita hapo. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana, niwakumbushe maswali mafupi, majibu mafupi. Mheshimiwa Maimuna Pathan.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, ni lini barabara ya kutoka Masasi kwenda Liwale kupitia Nachingwea itajengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara ya Masasi – Nachingwea – Liwale ni kati ya barabara saba ambazo zilichaguliwa kuingia kwenye mpango wa *EPC+F;* na tunavyoongea sasa hivi upande wa ufundi zimeshakamilishwa ziko kwenye upande wa fedha sasa ya kufanyiwa tathmini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Issaay swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Karatu – Mbulu kilometa 76 kama ilivyowekwa kwenye bajeti ya mwaka huu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zacharia Issaay, Mbunge wa Mbulu Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom – Sibiti ndiyo barabara ambazo kati ya zile barabara saba ipo kwenye mpango huu wa *EPC+F*. Kwa hiyo, kama itakavyokuwa imekamilika basi kilometa hizo 76 itakuwa ni sehemu ya ujenzi wa hiyo barabara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Catherine Magige swali la nyongeza.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Spika, wananchi wa Monduli wamekuwa wakipata changamoto kubwa ya barabara inayotokea Monduli Chini kwenda Monduli Juu nyumbani kwa Sokoine.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga barabara hii katika kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG.**

**GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Catherine Magige, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara zote ambazo ni za mkoa zinatakiwa zijengwe kwa kiwango cha lami, lakini kinacho gomba hapa ni bajeti kwa hiyo tunakwenda kwa awamu.

Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii kwa umuhimu wake pia ipo kwenye mpango lakini itaanza kujengwa pale ambapo bajeti itaruhusu. Ahsante

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamisi Taletale swali la nyongeza.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, je, ni lini Serikali itaenda kujenga barabara ya Bigwa – Kisaki ya kilometa 78 kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Taletale, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba barabara ilishatangazwa kwa ajili ya kuijenga na kwa hiyo sasa hivi ipo kwenye hatua ya manunuzi kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kasalali Mageni swali la nyongeza.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Barabara ya kutoka Haydom mpaka Katesh ni mwendelezo wa barabara ya kutokea Fulo au Bujingwa kupitia Nyambiti mpaka Mari ambayo imekuwa ikiahidiwa kujengwa kwa kiwango cha lami na Serikali kwenye ilani mbalimbali za uchaguzi; je, ni lini sasa barabara hii inaanza kujengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**N NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, kama nilivyosema barabara hii iko kwenye mpango wa kuijenga; kwa hiyo mara fedha itakapokuwa imepatikana barabara hii sasa tutaanza kuijenga kama tulivyoahidi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Samweli Hhayuma swali la nyongeza.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wananchi maneno ya usanifu wa kina au upembuzi yakinifu hawayaelewi vizuri;

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya Mogitu – Hydom kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, swali lililoulizwa na Mheshimiwa Hhayuma lilikuwa ndilo swali la msingi lililohusu Mogitu – Haydom na nimeshalijibu kwamba tayari mkandarasi yupo anafanya usanifu wa hiyo barabara tujue gharama halafu fedha itafutwe kwa ajili ya kuijenga, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Seif Gulamali swali la nyongeza.

**MHE. SEIF K. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana; je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa lami barabara ya Choma – Ziba – Nkinga – Simbo mpaka Puge?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara ya Choma – Puge ni barabara ambayo Mheshimiwa Mbunge amekuwa anaifuatilia sana. Hata hivyo, kwa kuwa bajeti bado hatujaiwasilisha naomba Mheshimiwa awe na subira tuone nini mwaka huu tutakuwa tumeipangia hiyo barabara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Simon Fiyao Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 10

**Ujenzi wa Bandari Kavu Tunduma**

**MHE. STELLA S. FIYAO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Bandari kavu katika Mji wa Tunduma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. FREDY A. MWAKIBETE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *(TPA)* imekamilisha zoezi la kufanya upembuzi yakinifu wa kuendeleza bandari kavu zote nchini ikiwemo ya Bandari Kavu ya Tunduma.

Mheshimiwa Spika, Kiuchumi na kibiashara, Bandari Kavu ya Tunduma ni muhimu sana kwa sababu ndilo langu kuu la kupitisha bidhaa za nchi za Zambia, DRC na nchi nyingine kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Bandari hiyo ina mvuto zaidi wa kibishara, mpango wa Serikali ni kushirikisha sekta binafsi ikiwa pamoja na halmashauri kwenye maeneo husika. *TPA* inaendelea na vikao vya wadau ili kushawishi uwekezaji huo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuwa na maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa Serikali imetambua uwepo na umuhimu wa Bandari Kavu ndani ya Mji wa Tunduma na tayari Halmashauri ya Mji wa Tunduma imetenga zaidi ya ekari 2,000 kwa ajili ya uwekezaji wa bandari kavu. Sasa nataka kujua je, ni sekta ngapi binafsi ambazo zimefikiwa mpaka sasa ili kuja kuwekeza bandari kavu ndani ya Mji wa Tunduma?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa Taifa sasa lipo katika ushindani wa kibiashara; je hatuoni kuchelewachelewa tunaweza tukaleta matokeo hasi? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI UCHUKUZI (MHE. FREDY A. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mbunge wa Viti Maalumu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Halmashauri ya Tunduma ina eneo la kuweza kujenga bandari hii kavu na sekta ambazo ziko tayari kwa ajili ya uwekezaji katika eneo hili la bandari kavu, kuna Sekta ya Kilimo, Sekta ya Viwanda na Sekta ya Mifugo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa swali lake la pili, suala la kuchelewachelewa. Kimsingi Serikali imechukua hatua za kuongea na watu binafsi na ndio maana hadi sasa tupo kwenye majadiliano ya mwisho ili eneo la Mpemba ambalo litakuwa linaunganisha upande wa Malawi pamoja na Zambia na DRC liweze kujengwa Bandari hii kavu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdul-Aziz Abood, swali la nyongeza.

**MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD:** Mheshimiwa Spika, Morogoro ina barabara mbili kuu zinazounganisha nchi za *SADC* na Afrika Mashariki. Morogoro ilitenga hekari 500 kwa ajili ya bandari kavu, je Serikali ina mpango gani wa kujenga Bandari Kavu katika Mji wa Morogoro?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI UCHUKUZI (MHE. FREDY A. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Abdul-Aziz, Mbunge wa Morogoro kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Morogoro pia tuna eneo kwa ajili ya ujenzi wa Bandari Kavu na kwa kuwa reli yetu *SGR* itaanza kazi hivi karibuni na katika mwaka wa fedha ujao nimwombe Mheshimiwa Mbunge apitishe bajeti yetu ya Wizara ya Ujenzi kwa kuwa ni miongoni mwa Bandari Kavu zitakazojengwa katika mwaka wa 2023/2024. Ahsante.

**SPIKA:** ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Nusrati Shaaban Hanje, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 11

**Mkopo wa wanafunzi wa Vyuo vya Kati Nchini**

**MHE. NUSRAT S. HANJE** aliuliza:-

Je ni lini Serikali itatoa mikopo kwa wanafunzi wa Vyuo vya Kati nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia naomba kujibu Swali la Mheshiwa

Nusrat Shaaban Hanje, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa elimu ya kati katika maendeleo ya nchi, Serikali imeendelea kugharamia uendeshaji wa vyuo vya kati kupitia ruzuku ambapo kwa mwaka 2022/2023, imetenga kiasi cha shilingi Bilioni 41.47 kwa wanafunzi 2,435 waliopo katika vyuo vya kati wanaosoma fani za sayansi na ufundi. Aidha, Serikali inakamilisha taratibu za kuwezesha mikopo kutolewa kwa ajili ya elimu ya kati.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nusrat Hanje, swali la nyongeza.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu hayo, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa mpaka sasa Serikali inatoa mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vitatu ambavyo ni vya Serikali *MUST, DIT* na *Arusha Technical College* ambao ni 2,435 pekee. Ni nini sasa maandalizi ya msingi ambayo Serikali imeshafanya mpaka sasa kuhakikisha kwamba inatoa mikopo kwa wanafunzi wote wa vyuo vya kati ikiwepo wa *private*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa nini sasa Serikali isione namna ambavyo inaweza kushirikisha Sekta Binafsi ikiwemo benki ili na wao waweze kushiriki katika kutoa mikopo kwa vyuo vya kati kwa riba nafuu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili

ya nyongeza ya Mheshimiwa Nusrat Hanje, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la kwanza anataka kufahamu maandalizi au mkakati wa Serikali kwa upande wa utoaji mikopo katika elimu ya kati. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, eneo la kwanza kama nilivyojibu kwenye swali langu la msingi, tumeendelea au tutaendelea kupeleka ruzuku kwenye vyuo hivi vya elimu ya kati kwa lengo la kuhakikisha kwamba kwanza tunaenda kushusha zile gharama za uendeshaji au ile gharama ya ada ambayo wanafunzi wanalipa.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, tulilofanya kama Serikali, Serikali tayari imeshafanya mabadiliko ya Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ili kuhakikisha sasa tunaenda vilevile ku-*cover* elimu ya kati. Kwa hiyo ile Sheria ya Bodi ya Mikopo nayo tayari tumeshaifanyia marekebisho.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu, Serikali inafanya mapitio ya uwezo wa Bodi ya Mikopo namna gani inaweza kuratibu utoaji wa mikopo katika vyuo hivi vya kati.

Mheshimiwa Spika, eneo la nne kama mkakati Wizara sasa inafanya tathmini ya fani gani ambazo tutaanza nazo kwa ajili ya utoaji wa mikopo katika eneo hili la elimu ya kati.

Mheshimiwa Spika, katika swali la pili, anataka kujua mkakati wa Serikali kuhususha Sekta Binafsi, tayari tumeshaanza majadiliano na Sekta Binafsi ikiwemo mabenki na naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari Benki ya *NMB* imetoa bilioni 200 kwa ajili ya mikopo hii ya Elimu ya Juu pamoja na kati na tunaendelea na juhudi hizo na wadau wengi wameonyesha nia ya kuunga mkono juhudi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya msingi nakala niliyonayo hapa mbele inasema kwa mwaka 2022/2023 iko sahihi au ni 2023/2024? Ni bajeti hii?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ndio ni bajeti hii ndio tulitenga hiyo bilioni 41.47 kwa ajili ya ruzuku siyo kwa ajili ya kutoa mikopo, hii ni ruzuku tunayopeleka.

**SPIKA:** Kwa hiyo hii imeshaanza kwenda?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ndio hii inakwenda kila mwaka, tumekuwa tukipeleka.

**SPIKA:** Haya ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Ameir Abdallah Ameir, Mbunge kutoka Baraza la wawakilishi sasa aulize swali lake. Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar atauliza kwa niaba yake.

Na. 12

**Mikakati inayotumiwa na Balozi za Tanzania kutangaza bidhaa za Tanzania Kimataifa**

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR K.n.y. MHE. AMEIR ABDALLAH AMEIR** aliuliza:-

Je, Balozi za Tanzania zinatumia mikakati gani kutangaza bidhaa za Tanzania Kimataifa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Mbarouk Mbarouk, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ameir Abdallah Ameir, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001 inatoa msisitizo katika utekelezaji wa diplomasia ya uchumi ambayo lengo kuu ni kujenga, kukuza na kuimarisha uchumi wa nchi yetu. Kwa muktadha huo, balozi zetu nje ya nchi, zimeendelea kubuni mikakati mbalimbali katika kutekeleza vyema diplomasia ya uchumi kwa kutangaza bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini ikiwa ni pamoja na masoko ya bidhaa na huduma hizo.

Mheshimiwa Spika, mikakati hiyo ni pamoja na kuratibu na kufanikisha upatikanaji wa vibali/ithibati kwa kampuni za Tanzania kuuza bidhaa zao katika masoko ya nje; kuratibu na kushiriki katika makongamano ya biashara, maonesho na mikutano ya kimataifa ndani na nje ya nchi; kuratibu na kufanikisha ziara za wawekezaji na wafanyabiashara kutoka nje ya nchi; Kuratibu na kufanikisha ziara za kuutangaza utalii *(road show)*, watu maarufu na mashuhuri, kampuni za kitalii na Kubidhaisha lugha ya Kiswahili na kuitangaza kimataifa, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar, swali la nyongeza.

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu haya mazuri, lakini pamoja na mjibu haya na jitihada hizi za Serikali kupitia juhudi hizi za Serikali ambazo zinafanyika kupitia Mabalozi wetu mbalimbali naomba kufahamu, ni bidhaa zipi hasa za kilimo ambazo zimetangazwa kupitia Mabalozi wetu na zimepata soko kubwa zaidi nje ya nchi yetu? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *list* hii ni kubwa sana, lakini itoshe tu kusema kwamba kwa mazao yanayoongoza ni parachichi, soya na mazao mengine kama vile matunda na mbogamboga, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maliasili na Utalii Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrew, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 13

**Mpango wa kutenga bajeti kwa hifadhi changa za utalii**

**MHE. JACQUELINE K. ANDREW** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutenga bajeti kwa Hifadhi changa za utalii ili kukuza utalii katika hifadhi hizo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Marry Masanja, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrew, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia fedha za Mpango wa Maendeleo na Mapambano dhidi ya UVIKO-19, tayari ilishaanza mchakato wa kuboresha hifadhi changa 17 za utalii ikiwemo kuboresha miundombinu ya barabara, huduma za malazi na chakula na maeneo ya uwekezaji ambapo tayari wawekezaji wameonesha nia ya kuwekeza. Hifadhi za Taifa changa zilizopo katika mkakati huo ni Burigi-Chato, Gombe, Ibanda-Kyerwa, Katavi, Kigosi, Kisiwa cha Rubondo, Kisiwa cha Saanane, Kitulo, Milima ya Mahale, Milima ya Udzungwa, Mikumi, Mkomazi, Mto Ugalla, Nyerere, Ruaha, Rumanyika-Karagwe na Saadani.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuboresha hifadhi hizo kwa lengo la kukuza utalii na kuongeza mapato. Maboresho hayo yanaenda sambamba na utekelezaji wa Programu ya Tanzania, *the Royal Tour* ambapo kwa sasa Serikali imejikita zaidi kwenye maeneo mapya ya utalii zikiwemo hifadhi hizo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jacquiline Kainja, swali la nyongeza.

**MHE. JACQUELINE K. ANDREW:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili. Swali langu la kwanza; katika mikoa yetu ambayo ina hifadhi changa, Wakuu wetu wa Mikoa wamejitahidi kujitokeza

kuhakikisha wanatangaza utalii katika hifadhi hizi changa. Je, Serikali ina mpango gani katika kuhakikisha inasaidia viongozi hawa wa mikoa ili kuweza kukuza utalii katika hizi hifadhi changa na tukizingatia bado miundombinu ni mibovu, magari pia hayatoshi, wanapata wakati mgumu hasa wanapokuwa wanafanya kazi za kutangaza hifadhi hizi kujikuta sasa inabidi waazime magari kutoka sehemu zingine, tunaonaje kama Serikali tuweze kusaidia kutangaza sekta hii ya Maliasili na Utalii?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; bado tunachangamoto nyingi kwenye upande wa ajira. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha ajira zinapatikana na kukuza sekta hii ya utalii hasa katika hifadhi hizi changa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jacquiline Kainja, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali kwa sasa imejikita katika maeneo mapya ya utalii zikiwemo hifadhi hizi ambazo imezitaja na malengo makuu ni kuhakikisha kwamba tunapanua wigo wa namna ambavyo watalii wataweza kufika katika maeneo hayo. Mikoa yote ya Tanzania tumeendelea kuwahimiza waendelee kuhamasisha utalii ikiwemo utalii wa ndani lakini pia tumejikita kuboresha miundombinu zikiwemo barabara, maeneo ya malazi na chakula ili sasa iwe rahisi kwa watalii kuweza kufika katika maeneo hayo. Kwa hiyo tunaendelea kuwahimiza Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya waendelee kuhamasisha masuala mazima ya utalii.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ameongelea kuhusu ajira. Tumeendelea kuwasiliana na Ofisi ya Rais, Menejimenti Utumishi na Utawala Bora kuangalia namna ya kuongeza watumishi ambao tutawasambaza katika maeneo mapya yaliyoko katika hifadhi hizo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, Mbunge wa Bagamoyo, sasa aulize swali lake.

Na. 14

**Gawio la Utalii lililotolewa na Eneo la Utalii Kaole kwa mwaka 2020/2021 na 2021/2022**

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE** aliuliza:-

Je, kwa mwaka 2020/2021 na 2021/2022 ni kiasi gani cha gawio kimetolewa na eneo la Utalii Kaole kwa Halmashauri ya Bagamoyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, Mbunge wa Jimbo la Bagamoyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Magofu ya Kaole kilianza kutambuliwa na kuhifadhiwa kisheria mwaka 1937 ilipoanzishwa Sheria ya Uhifadhi wa Majengo ya Kihistoria, kipindi cha utawala wa Mwingereza na kwa sasa yanalindwa kwa Sheria ya Mambo ya Kale, Sura 333. Hapo awali vituo vya mambo ya kale vilitumika zaidi katika masuala ya tafiti na

elimu hivyo kutembelewa zaidi na wanafunzi wa shule za msingi, sekondari na vyuo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na miongozo iliyopo hakuna gawio lolote linalotolewa kwa Halmashauri kutokana na mapato ya vituo vya malikale. Aidha, Magofu ya Kaole yanatoa fursa kwa wananchi wa Halmashauri ya Bagamoyo kunufaika kiutalii kwa kuuza bidhaa mbalimbali kwa watalii kama vile vitu vya kiutamaduni, vyakula na kutoa huduma ya malazi. Kwa kufanya hivyo, halmashauri hunufaika kupitia tozo mbalimbali kwa wafanyabiashara hao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, swali la nyongeza.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je Serikali haioni iko haja sasa ya kuondoa hizo sheria, miongozo na kanuni ili wananchi wa Kaole waweze kupatiwa gawio kwa kile ambacho kipo katika mji wao?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je ni lini Serikali sasa ina mpango wa kuwatumia wazee wa Kaole kuelezea historia ya magofu ya kale pamoja na kaole kwa wageni wanaokuja badala ya kuwatumia waajiriwa ambao historia hiyo wameisoma kwenye vitabu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante na naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mharami Shabani, Mbunge wa Bagamoyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa namna ambavyo sasa hivi Wizara ya Maliasili na Utalii makusanyo yake yanaenda Mfuko Mkuu hatuoni haja ya kurekebisha sheria hii kwa sababu makusanyo yote yanayokusanywa yanaenda Mfuko Mkuu na yanapofika kwenye Mfuko Mkuu, halmashauri zinapokea ruzuku mbalimbali ambazo zinatoka katika Mfuko Mkuu. Kwa hiyo fedha yote inayokusanywa katika maeneo haya tuna uhakika kwamba inaenda kulenga wananchi wa Tanzania nzima kutokana na masuala mazima ya utalii.

Mheshimiwa Spika, hili lingine alilosema la kutumia wazee tunalipokea, tutawashirikisha wazee wa Bagamoyo pamoja na maeneo mengine zilipo malikale ili tuweze kuipata historia kamili ya Tanzania pamoja na wazee wetu waliotutangulia, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 15

**Kuwezesha Vikundi vya Vijana na Wanawake kufanya uvuvi wa vizimba Ziwa Victoria**

**MHE. AGNES M. MARWA** aliuliza:-

Je, ni vikundi vingapi vya wanawake na vijana vimewezeshwa kufanya uvuvi wa vizimba Ziwa Victoria?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na kabla sijajibu swali, naomba kwa kifupi sana nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Rais ameweka mtu sahihi, mahali sahihi na kazi itafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi *(FETA)* Nyegezi Mwanza ilitoa mafunzo ya ufugaji samaki kwa vizimba kwa vijana 288 (wanaume 208 na wanawake 80). Vijana hao walitoka katika Wilaya za Nyamagana – 74; Ilemela – 54; Magu – 31; Misungwi – 21; Ukewere – 51; Sengerema - 28 na Buchosa - 29.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/2023, Serikali imetenga shilingi bilioni 20 kwa ajili ya kuwawezesha wakuzaji viumbe maji nchini. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 15.1 zitatolewa kwa wafugaji samaki kwa vizimba katika Ziwa Victoria kama mikopo ya pembejeo kwa masharti nafuu kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania *(TADB)*. Jumla ya wananchi 3,154 wanatarajiwa kunufaika kwa kupata mikopo ya vizimba, vifaranga na chakula cha samaki. Kati ya hao vijana ni 241, wanawake 290 na kampuni mbili za wanawake. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa swali la nyongeza.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Spika, je, ipo ruzuku ama mikopo nafuu ya kuwezesha miradi hii ya vizimba ili kufanya uvuvi kuwa wa kisasa zaidi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, Wizara ina mpango gani wa kuendelea kutoa elimu kuwawezesha wavuvi au wananchi wanaozunguka Ziwa Victoria kuwa na uelewa zaidi na haswa Mkoa wa Mara ambao bado hawajapata elimu hiyo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Mara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, natambua kwamba Mheshimiwa Mbunge ni mvuvi na ni Mchuuzi na ni mtu ambae anaipenda sana hiyo kada. Nimhakikishie tu kwamba Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi tunazo fedha ambazo ni za masharti nafuu kwa ajili ya wafugaji wa samaki kwa vizimba kwa vijana. Eneo la pili ni kwamba mpango wa kutoa elimu upo na sasa hivi tumeanza na programu za vijana atamizi ambao wanakuwa wakifundishwa juu ya ufugaji wa samaki na elimu ya viumbe maji katika maeneo ambayo yanazungukwa na bahari, maziwa ambapo vijana wengi wanahusika na kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, hivyo nimhakikishie tu Mheshimiwa Agnes Marwa kwamba kazi hiyo itafanyika. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Ikupa swali la nyongeza.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa fursa; nini mkakati wa Serikali kutoa kipaumbele kwa vijana wenye ulemavu wenye sifa kwenye mradi huu wa uvuvi wa vizimba? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Stella Ikupa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango na katika mipango yetu tumewapa vipaumbele watu wote wenye ulemavu na katika elimu ambayo tunaitoa sasa hivi moja wapo ya kigezo ni kuwa na wavuvi ambao wanatokana na watu wenye mahitaji maalum, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu, sasa nilete tangazo nililonalo hapa mbele, ninalo tangazo la wageni waliokuja Bungeni siku ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza kuna mgeni mmoja ambaye yuko Jukwaa la Spika na huyu ni mgeni wa Mheshimiwa David Kihenzile, Mkuu wa Wilaya ya Itilima kutoka Mkoani Simiyu Mheshimiwa Faidha Selemani Salehe, karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, vilevile tunao wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge kwanza ni wageni 44 wa Mheshimiwa Ritta Kabati ambao ni viongozi wa Kanisa na Kwaya ya Unabii kutoka *AICT* Dayosisi ya Kati, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni 25 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni wanamaombi kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wageni 27 ambao ni Wanachuo Seneti ya Vyuo Vikuu kutoka Jijini Mwanza, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndio wageni tuliyonao leo hapa Bungeni. Sasa tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI-** ***Ndc*** **– KATIBU WA BUNGE:** Uchaguzi wa Wenyeviti wa Bunge.

## UCHAGUZI WA WENYEVITI WA BUNGE

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwenye ratiba yetu ama kwenye orodha ya siku ya shughuli za siku ya leo tunao uchaguzi wa Wenyeviti wa Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, kama inavyoonekana kwenye orodha ya shughuli za leo, kuna shughuli ya Uchaguzi wa Wenyeviti wa Bunge na Kanuni ya Saba ya Kanuni za Bunge imeweka uwepo….

Waheshimiwa Wabunge mnaozungumza sijajua na ninyi kama mmesimama ama mmekaa, tusikilizane.

Kanuni ya Saba ya Kanuni za Bunge imeweka uwepo wa Wenyeviti watatu wa Bunge ambao huongoza vikao kwa utaratibu na maelekezo ya Spika au Naibu Spika kwa mujibu wa kanuni. Utaratibu wa kuwapata wagombea wa nafasi ya Wenyeviti wa Bunge umewekwa katika Kanuni ya 13, mchakato husika unaanza kwa Kamati ya Uongozi kupendekeza majina yasiyozidi sita kutoka miongoni mwa Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za

Bunge kwa kuzingatia Jinsi na pande za Muungano, baada ya hapo majina hayo hupelekwa Bungeni ili Bunge lipigie kura majina matatu.

Waheshimiwa Wabunge, katika kutekeleza masharti ya Kanuni ya 13 na taratibu zetu, Jumatatu siku ya tarehe 3 Aprili, 2023 Kamati ya Uongozi ilikutana na kwa kauli moja ilipendekeza majina matatu ili yaweze kuwasilishwa Bungeni na Bunge liombwe kuyathibisha.

Waheshimiwa Wabunge, majina ya Wabunge waliyopendekezwa na Kamati ya Uongozi ni kama ifuatavyo; Mbunge wa kwanza ni Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum, ahsante sana. Huyu ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii. *(Makofi)*

Mbunge wa pili ni Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini, huyu ni Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo. *(Makofi)*

Mbunge wa tatu Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini, ahsanteni sana. Haya huyu ni Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Bunge letu lilikwishaweka utaratibu kwamba katika chaguzi zinazofanyika hapa Bungeni, iwapo idadi ya wagombea inalingana na nafasi zilizopo na vigezo vinavyohitajika vimetimizwa basi wagombea hapo wanapita bila kupingwa. Utaratibu kama huu ulitumika kwenye Uchaguzi wa Wenyeviti wa Bunge katika Bunge la Kumi, Bunge la Kumi na Moja na katika Bunge hili la Kumi na Mbili ambapo Kamati ya Uongozi ilipendekeza majina matatu na baadae majina hayo yalithibishwa na Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa nafasi zilizopo za Wenyeviti wa Bunge ni tatu na kwa kuwa Kamati ya Uongozi imependekeza majina matatu Bunge hili katika Kikao cha leo Jumanne tarehe 4 Aprili, 2023 linaombwa kuwathibitisha Wabunge hao kuwa Wenyeviti wa Bunge. Ili kupata uamuzi wa Bunge na sasa nitawahoji kama ifuatavyo:-

Waheshimiwa Wabunge wanaoafiki kwamba Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile na Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, wathibitishwe kuwa Wenyeviti wa Bunge waseme ndiyo.

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Wasioafiki kwamba Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile na Mheshimiwa Daniel Baran Sillo wathibitishwe kuwa Wenyeviti wa Bunge waseme siyo.

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani waliyosema ndiyo wameshinda. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii sasa kuwatangaza kwamba Wabunge hao watatu, kwa maana ya Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile na Mheshimiwa Daniel Baran Sillo ndiyo Wenyeviti wa Bunge. Sasa kwa sababu ya hapa wamethibitishwa hawajapata nafasi ya kujieleza nitampa kila mmoja wao dakika tatu za kuwashukuru Wabunge kwa kuwakubali.

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, dakika tatu. *(Makofi)*

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi ya hii ambayo umenipa. Natumia fursa hii kwanza kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambae ni muweza wa kila jambo, pia nitumie fursa hii pia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge na Kamati ya Uongozi wote kwa namna ambavyo mmeniamini kwa mara nyingine ili niweze kuwa Msaidizi wako katika nafasi hii ya Mwenyekiti nikishirikiana na wenzangu. Kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu naamini kabisa kwamba atanisaidia tena niweze kufanya kazi kama ambavyo nimefanya kipindi kilichopita, kwa hivyo ninawaomba nanyi ushirikiano wenu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile dakika tatu.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kukushukuru wewe Kiongozi Mkuu wa Muhimili, kwanza kwa malezi yako katika kipindi kilichopita nikiwa Mwenyekiti wa Bunge lakini pili kwa imani yako katika hatua hii pia niwashukuru Wabunge wenzangu wote kwa kuniamini na kunithibisha kwa nafasi hii ya Mwenyekiti wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, bila kusahau na kwa umuhimu mkubwa sitaacha kushukuru Chama changu cha Mapinduzi chini ya Mwenyekiti wetu Rais Samia ambaye ndiye kupitia kwao naweza kupata fursa kuendelea kuwa kwenye nafasi hizi.

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana ninawaahidi ushirikiano, unyenyekevu na utiifu mkubwa katika kuitumikia nafasi hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, dakika tatu.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutuweka salama na kukutana siku hii mbele ya Bunge letu Tukufu vilevile nishukuru sana chama chetu, Chama cha Mapinduzi kwa kuniamini kwa nafasi hii. Nichukue nafasi hii kuipongeza pia Kamati ya Uongozi kwa kutupitisha na kutuamini na Waheshimiwa Wabunge wote ninawaahidi tu ushirikiano na niombe ushirikiano kutoka kwenu ili tuweze kutetea jukumu letu hili la kumsaidia Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Naibu Spika katika uendeshaji wa Bunge letu tukufu.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wajumbe nawashukuru sana naombeni sana ushirikiano wenu, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsanteni sana. Waheshimiwa Wabunge, nitumie sasa fursa hii kuwapongeza sana Wenyeviti wetu wapya watatu ambao watatusaidia Spika na Naibu Spika katika kufanya kazi iliyo mbele yetu hasa kipindi hiki cha Bunge la Bajeti lakini na Mabunge yatakayokuja huko mbele, tunaamini ushirikiano ambao mmekuwa mkitupatia sisi na wao mtawapa vivyo, natoa pongezi hizi kwa niaba ya Wabunge wote Wenyeviti mlioshinda msije mkaanza fulani hajanipongeza ndiyo tumeshawapongeza Bunge zima kwa ninyi kuwa Wenyeviti wa Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu. Tunayo mambo mawili bado lakini tuanze na moja la kutengua Kanuni. Nimuite Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama. *(Makofi)*

## HOJA YA KUTENGUA KANUNI

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA BUNGE NA URATIBU):** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza toka Mheshimiwa Rais ilivyompendeza kufanya mabadiliko ya Baraza la Mawaziri, naomba uniridhie nimshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kuendelea kuniamini kumsaidia katika majukumu yake na kuja kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa Bunge la Jamhuri ya Muuungano wa Tanzania ili kuweza kutekeleza majukumu yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, kwa mujibu wa Kanuni ya 34(2) na (4), Bunge linakutana hadi Saa 7:00 na kusitishwa mpaka saa 11.00 jioni na baada ya hapo Bunge huendelea kukaa mpaka saa 1:45 usiku ambapo Mheshimiwa Spika husitisha shughuli na kulihairisha Bunge hadi siku nyingine;

Na kwa kuwa, katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge unaoanza leo waumini wa dini ya kiislamu wamo kwenye Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan ambapo katika kipindi hicho hutakiwa kuswali na kufuturu kila siku ifikapo saa12:30 jioni. Aidha, waumini wa dini ya kikristo wanamalizia kipindi cha Kwaresma;

Na kwa kuwa, ili kuliwezesha Bunge kutekeleza shughuli zake zilizopangwa kikamilifu na kwa wakati huo huo kuwezesha Waheshimiwa Wabunge wa dini zote kuswali, kusali na kufuturu kwa wakati muafaka kwa mujibu wa taratibu za dini zao, inabidi Bunge litengue Kanuni ya 34(2) na (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 174(1);

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba kwa madhumini ya utekelezaji bora wa shughuli za Bunge wakati huu wa kipindi cha Kwaresma na kipindi cha Mfungo wa Mwezi

Mtukufu wa Ramadhan; moja, Kanuni ya 34(2) ambayo inaelekeza kwamba Bunge litakutana hadi saa 7.00 mchana ambapo Spika atasitisha shughuli yoyote itakayokuwa inafanyika hadi saa 11.00 jioni itenguliwe na badala yake Bunge linapositishwa saa 7.00 mchana liendelee na shughuli ifikapo saa 10.00 jioni badala ya saa 11:00 jioni. Kanuni ya 34(4) ambayo inaelekeza kwamba Bunge litaendelea kukaa hadi saa 1.45 usiku ambapo Spika atasitisha shughuli na kuliahirisha hadi kesho yake itenguliwe, na badala yake Bunge liahirishwe ifikapo saa 12.00 jioni. Utaratibu huu utatumika wakati wa Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan tu na baada ya mfungo huo kukamilika Bunge litarejea katika utaratibu wake wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono lakini nimeona Wabunge wengine mmekaa, hii siyo hoja ya Serikali, hii ni hoja inayohusu kila mmoja aliyepo humu ndani. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji Hoja ya Kutengua Kanuni kama ilivyosomwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo tutakuwa tukifuata muda ule ambao tumekubaliana kwa maana ya kwamba kipindi cha mchana Bunge litaanza saa 10.00 jioni na kuisha saa 12.00 jioni.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**AZIMIO LA BUNGE**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Azimio la Bunge litaletwa kwetu na Mheshimiwa Mhandisi Ezra Chiwelesa.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 61(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha hoja kwamba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Azimio la Bunge la kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuimarisha demokrasia nchini na kukuza diplomasia ya uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kuruhusu na kunipa fursa hii adhimu ya kuwasilisha hoja hii ya azimio hili. Naomba pia kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi bora na thabiti aliyouonesha kwa taifa letu tangu alipoingia madarakani. Nawaomba Watanzania wenzangu tuzidi kumwombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kumpa afya njema ili aweze kutekeleza majukumu haya ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sote tulishuhudia katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hali ya demokrasia na utawala bora imeendelea kuimarika nchini.

Miongoni mwa mambo muhimu yaliyochangia kuimarika kwa demokrasia ni pamoja na haya yafuatayo:-

(1) Uamuzi wa kuruhusu shughuli za siasa hasa mikutano ya hadhara kufanyika nchini kote; uamuzi huu umefufua na kuimarisha shughuli za siasa nchini, kwani vyama vya siasa vimepata fursa ya kunadi sera zao na kutoa mawazo mbadala ambayo yatasaidia Serikali kutekeleza huduma za kijamiii na kiuchumi hususan masuala yanayogusa maendeleo ya wananchi;

(2) Kuanzisha vikao vya maridhiano ya kisiasa miongoni mwa vyama vya siasa nchini ili kuhakikisha kunakuwepo mahusiano mema miongoni mwa makundi ya kisiasa yaliyokuwa yanahasimiana;

(3) Kuanzisha mchakato wa kufanya marekebisho ya kimfumo na kisheria yanayoongoza shughuli za kisiasa na kudumisha misingi ya amani na mshikamano miongoni mwa Watanzania; na

(4) Kuridhia kuundwa kwa kikosi kazi cha kufanyia kazi masuala yananyohusu demokrasia ya vyama vingi vya siasa nchini ambapo lengo kubwa la kikosi kazi hicho ilikuwa ni kupendekeza namna bora ya kutekeleza haki ya vyama vya siasa ikiwemo kuwepo na uwanja sawa wa kufanya shughuli za kisiasa bila kukiuka sheria na maadili ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tumeshuhudia ukuaji mkubwa wa diplomasia ya uchumi ambapo Mheshimiwa Rais mwenyewe amekuwa chachu ya mafanikio hayo kwa kuwa mwanadiplomasia mahiri. Katika kipindi hicho, tumeshuhudia nchi yetu ikipitia mafanikio haya yafuatayo:-

(1) Kuongezeka kwa masoko ya bidhaa zinazozalishwa nchini katika masoko ya nje;

(2) Kuimarika kwa mahusiano ya kimkakati na makampuni ya kimataifa yanayolenga kuwekeza katika sekta za uzalishaji ili kuchochea uchumi wa nchi yetu;

(3) Kuwezesha upatikanaji wa misaada na mikopo ya masharti nafuu kutoka kwenye taasisi za fedha duniani ambapo kwa kiasi kikubwa imesaidia kuboresha shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwemo elimu, miundombinu, afya na maji.

(4) Kukua kwa shughuli za uwekezaji na kuongezeka kwa idadi ya wawekezaji wapya nchini kutoka nje ya nchi, baada ya kufanyika maboresho ya mazingira ya kufanya biashara nchini;

(5) Kupitia filamu maarufu ya Tanzania *The Royal Tour* amefanikiwa kutangaza vivutio vilivyoko nchini na hivyo kukuza sekta ya utalii ambapo tumeshuhudia watalii maelfu kwa maelfu wakiingia nchini na hivyo kuongeza pato la Taifa; na

(6) Kuimarika kwa mahusiano na mataifa mengine na taasisi za kimataifa kutokana na ziara mbalimbali ambazo Mheshimiwa Rais amezifanya nje ya nchi ambazo zimezaa matunda makubwa. Mathalan, hivi karibuni nchi yetu imepokea ugeni mkubwa wa Mheshimiwa Kamala Harris, Makamu wa Rais wa Marekani. Kupitia ziara hiyo, Serikali ya Marekani imeahidi kuimarisha ushirikiano na Tanzania kwenye sekta mbalimbali ikiwemo miundombinu, viwanda, usalama wa mitandao, TEHAMA, afya usafirishaji na usalama wa chakula.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa niwasilishe Azimio la Kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuimamrisha demokrasia nchini na kukuza diplomasia ya uchumi kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameonesha wazi nia yake ya kuifanya Tanzania kuwa moja, salama na bila kundi lolote kuwa nyuma katika kufurahia demokrasia ya kweli;

Na kwa kuwa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa mstari wa mbele katika kukuza na kuimarisha diplomasia ya uchumi ambayo imelenga kuiletea Taifa letu maendeleo;

Kwa hiyo basi, Bunge hili katika Mkutano wake wa Kumi na Moja, Kikao cha Kwanza, tarehe 4 Aprili, 2023, linaazimia kwa dhati na kauli moja haya yafuatayo:-

(a) Kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuimarisha demokrasia nchini; *(Makofi)*

(b) Kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukuza demokrasia ya uchumi; na *(Makofi)*

(c) Kumuunga mkono Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika majukumu yake ya kazi ya Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, kumwombea afya njema, baraka na ulinzi wa Mwenyezi Mungu katika kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, sasa tutaendelea na utaratibu wetu. Ahsanteni sana.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Sasa kwa utaratibu wetu, watu mbalimbali huomba kuchangia, na hapa mbele ninayo maombi tayari ya Waheshimiwa Wabunge kadhaa ambao wameomba kuchangia. Kwa hiyo, tutawapa nafasi hao wachangie halafu mtoa hoja ya hili azimio atakuja kuhitimisha.

Tutaanza na Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Tadayo, na Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka ajiandae.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia katika azimio la kumpongeza Mheshimia Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan.

**SPIKA:** Samahani, Mheshimiwa Neema, uchangiaji itakuwa dakika tano.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia azimio hili la kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mtakubaliana nami katika kipindi hiki cha miaka miwili Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameonesha wazi dhamira yake ya kusimamia misingi ya haki za binadamu, utawala bora, demokrasia, pamoja na diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la haki za binadamu, nampongeza sana Mhehimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuruhusu mikutano ya hadhara, kufungulia

vyombo vya habari vilivyokuwa vimefungwa, kukubali kufanya maboresho ya sheria za huduma za vyombo vya habari na tayari rasimu iko wazi, kusema hadharani kuhusu kutoridhishwa na upatikanaji wa Haki Jinai na kuunda Tume ya Haki Jinai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika katika eneo la utawala bora, nampongeza sana Mhehimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika hotuba yake aliyowasilisha wiki iliyopita kwenye Mkutano wa *Summit for Democracy,* ameiambia dunia kwamba Tanzania itarudi kujiunga katika *OGP (Open Government Partnership)*. Hii ni hatua muhimu sana kwa sababu msingi wa *OGP* ni kuimarisha Serikali ambazo zinafanya kazi kwa uwazi, uwajibikaji na kuwainua wananchi kuweza kuwajibisha Serikali. Kwa kitendo hiki itaongeza imani kwa wawekezaji wakubwa ambao wanapenda kuwekeza kwenye nchi ambazo zina mifumo thabiti ya utawala bora na sera ambazo zinatabirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika eneo la demokrasia, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuimarisha demokrasia hapa nchini kwetu. Alianza hivyo kwa kuunda kikosi kazi ambacho kimemshauri katika maeneo ya demokrasia ya vyama vingi vya kisiasa na mengi ambayo amependekeza, tayari ameshaanza kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikirejea tena katika hotuba yake ya wiki iliyopita katika Mkutano wa *Summit for Democracy*, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameahidi kwamba Sheria ya Vyama vya Siasa inakwenda kuboreshwa, Sheria ya Taifa ya Uchaguzi inakwenda kuboreshwa na mchakato wa Katiba Mpya unakwenda kuanzishwa. Nami naamini kupitia yote haya, moja ya azma yake kubwa ya kuimarisha ushiriki na ushirikishwaji wa wanawake katika siasa na wenyewe utakwenda kuimarishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha katika eneo la dipolmasia ya kiuchumi, wote mtakubaliana nami kwamba katika miaka hii miwili Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameifungua nchi yetu. Katika kipindi cha miaka miwili, kupitia ziara alizofanya nje ya nchi, tumeweza kupata miradi yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 793 ambayo imesajiliwa *TIC*. Hilo ni jambo kubwa sana la kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vivyo hivyo, hivi karibuni tumepata ugeni wa Makamu wa Rais wa Marekani Mheshimiwa Kamala Harris, na kupitia ugeni wake Tanzania imeweza kupata msaada wa kifedha wa jumla ya Dola za Kimarekani milioni 560 ambayo ni sawasawa na takribani shilingi trilioni 1.3.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, inaonesha ni namna gani ambavyo kuna umuhimu mkubwa wa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan aendele kufanya ziara nje ya nchi kwa sababu ziara hizi zinapata tija na sisi ambao tunapata nafasi mbalimbali za kushiriki mikutano ya nje ya nchi, tunajisikia fahari sana pale ambapo tunajitambulisha tunatoka Tanzania. Nasi tunafuata nyayo zake za kuhakikisha kwamba fursa yoyote ambayo tunaipata tunaisemea vizuri nchi yetu na tunatafuta fursa mbalimbali za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja na naomba niungane na Wabunge wenzangu wote na Watanzania wote kumuunga mkono na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa mageuzi makubwa anayoyafanya katika eneo la haki za binadamu, eneo la utawala bora, eneo la demokrasia na eneo la diplomasia ya uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Tadayo, atafuatia na Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, na Mheshimiwa Mbarouk Nassor Mbarouk ajiandae.

Waheshimiwa Wabunge, hili azimio limeshawekwa kwenye vishikwambi vyenu. Mheshimiwa Joseph Tadayo.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Spika, nami nashukuru sana kupata fursa hii ya kuchangia azimio hili muhimu. Historia inajieleza kwamba nchi yetu toka ipate uhuru imekuwa mstari wa mbele katika kusimamia ajenda zilizoko mezani mwa Afrika na dunia kwa ujumla katika maeneo ya uchumi, siasa na maeneo ya kijamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru Mungu kwamba katika awamu hii ya sita tumepata kiongozi ambaye anayatambua haya na yuko tayari kuyaishi. Sote ni mashahidi kama mtoa hoja alivyozungumza kwamba Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imefanya juhudi za makusudi kuhakikisha kwamba demokrasia na utawala bora vinastawi katika nchi yetu. Sasa hii ni muhimu katika kuleta utengamano na amani ndani ya nchi, lakini pia katika kukuza uchumi.

Mheshimiwa Spika, hakuna nchi ambayo inaweza ikakua kiuchumi kama hakuna demokrasia na utawala bora kama ambavyo sasa hivi hapa Tanzania tulivyo. Tunao ushahidi kabisa wa nchi nyingi ambazo zina uchumi mkubwa sana wa maliasili na kila kitu, lakini kwa sababu hakuna amani na utulivu, uchumi ule na zile mali haziwafai kitu chochote kw kuwa amani na utulivu unakuja pale ambapo kuna demokrasia, utawala bora na haki. Kwa hiyo, kwa hilo lazima tumpongeze sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa diplomasia ya kiuchumi, kwanza pamoja na maana zake nyingine nyingi,

lakini diplomasia ya uchumi ni zile hatua za makusudi ambazo Taifa linazichukua ili kuonesha mahusiano mazuri na dunia na pia kukuza uchumi na ajira za wananchi wake bila kujali kama kuna gharama zozote za kisiasa ambazo zinaingia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika nchi yetu tumeona faida kubwa sana ya diplomasia ya kiuchumi ambayo Mheshimiwa Rais ameisimamia. Majimboni kwetu kote kuanzia Jimboni kwangu Mwanga na Waheshimia Wabunge wote wanashuhudia kwamba iko miradi mikubwa ambayo inaendelea kuliko kipindi kingine chochote ambacho kimewahi kuwepo katika historia ya nchi yetu. Hii miradi inaendelea, mingine kutaokana na fedha ambazo zinatoka nje na pia hali ya uchumi inaimarika kutokana na utawala bora na hali ya demokrasia ambayo tunayo katika nchi.

Mheshimiwa Spika, kubwa la kumpongeza Mheshimiwa Rais ni kwamba amesisitiza kabisa masuala haya ya demokrasia, utawala bora na haki za binadamu kwamba yatafanyika kwa kuzingatia mila na desturi zetu sisi Watanzania. Hatuingii katika masuala haya kwa lugha za mitaani kusema kichwa kichwa, bila kuangalia kwamba sisi Watanzania tumetoka wapi na historia yetu imetoka wapi? Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais anatuongoza vizuri kwamba tuingie kwenye mambo haya ambayo ni muhimu katika dunia, lakini kwa kuzingatia mila zetu na desturi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni rahisi sana watu kusema kwamba aah, mbona haya mambo tayari yapo kwenye Katiba! Ni sahihi, yapo kwenye Katiba, hata hivyo zipo nchi nyingi ambazo mambo yapo kwenye Katiba za nchi zao lakini wanakosa viongozi ambao wana utashi wa kuyatekeleza na kuyasimamia, na hiyo hasa ndiyo sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa uchache tu kwa kweli niungane mkono na mtoa hoja pamoja na Waheshimiwa Wabunge wenzangu na kuomba kwamba tumuunge mkono Mheshimiwa Rais katika hili na Tanzania kwa ujumla katika hatua hizi za utekelezaji wa sera hizi za kidemokrasia, utawala bora na diplomasia ya kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka atafuatiwa na Mheshimiwa Mbarouk Nassor Mbarouk na Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, ajiandae.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi ya kwanza kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuungana na Wabunge wenzangu katika azimio hili muhimu sana ambalo Bunge hili limeiamua katika siku yetu ya leo ya mkutano huu.

Mheshimiwa Spika, Waswahili wanasema, "*chanda chema, huvishwa pete.*" Nachukua nafasi hii kuwapongeza waliowaza na kuleta pendekezo hili la kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa aliyoifanyia nchi yetu Afrika na dunia katika muda mfupi wa uongozi wake.

Mheshimiwa Spika, natoa azimio la kumpongeza Rais kutokana na kazi kubwa aliyoifanya kuimarisha demokrasia nchini. Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Awamu ya Sita anafanya haya tukijua dhahiri kwamba amesimama katika mabega ya mafanikio makubwa ya waliomtangulia kuanzia Baba wa Taifa hadi Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, kwa maana ya awamu zote zilizomtangulia.

Mheshimiwa Spika, awamu zilizotangulia ziliweka rekodi ya Tanzania katika hali ya juu sana katika suala zima la demokrasia na diplomasia. Hakuna asiyejua kazi nzuri iliyofanywa na Mheshimiwa Dkt. Salim Ahmed Salim na kuiweka Tanzania katika ramani ya dunia; na hakuna asiyejua kazi nzuri iliyofanywa na Mheshimiwa Asha Rose Migiro akiiwakilisha nchi hii na kuwa mwanamke wa kwanza na Mtanzania wa kwanza kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba kazi nzuri inayofanywa na mwanadiplomasia namba moja Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuendeleza kazi nzuri iliyoasisiwa na waasisi wa Taifa hili na ameifanya kwa kasi ambayo hakuna mfano wake. Katika muda mfupi wa kazi aliyoifanya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameimarisha demokrasia, demokrasia ambayo inazingatia misingi ya utu, misingi ya usawa, misingi ya haki katika nchi hii, bara hili na hata alipokwenda kuhutubia Umoja wa Mataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amethibitisha hayo alipozungukia mataifa ya jirani kuweka mahusiano mema kati ya Tanzania na nchi zinazotuzunguka, yeye mwenyewe kwa kutembelea mataifa hayo. Leo Tanzania katika nchi zinazituzunguka, watu wanatuzungumza vizuri.

Mheshimiwa Spika, Rais pia kwa kujua diplomasia ya kimataifa inahitaji wawakilishi wa nchi wenye weledi na uelewa mkubwa, amehakikisha kwamba anawateua mabalozi ambao wana ufahamu juu ya sera, juu ya mipango ya nchi yetu, juu ya fursa zilizoko duniani, na hii imewezesha mabalozi hao kutekeleza na kuendeleza kazi nzuri aliyoianzisha katika filamu yake ya *Royal Tour* na tumeshuhudia wawekezaji wengi wakija katika nchi yetu,

tumeshuhudia pia wafanyabiashara wetu wakiungana na dunia nzima katika tasnia ya biashara. Waswahili wanasema, "*Ukiona vyaelea, ujue vimeundwa.*" Haya yamefanikiwa kutokana na kazi nzuri aliyoianzisha, siyo mwingine bali ni Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi Watanzania na hasa tukiongozwa na Bunge lako Tukufu na wewe mwenyewe kutuongoza, tuna kila sababu ya kusimama kifua mbele na kwa hakika kutoa matamko ya dhahiri ya kumuunga mkono Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa sababu ameirudisha Tanzania mahali tulikokuwa tunaijua huko, na ndiyo maana hata katika kipindi hiki ambacho dunia imetikisika kutokana na tatizo la Uviko, Tanzania tumeendelea kuwa na uwezo wa kuendeleza miradi ya kimkakati, tumeendelea kuwa na uwezo wa kuweza kujenga shule zetu, zahanati zetu katika sekta zote; barabara na miundombiu mbalimbali. Hii ni matokeo ya kazi nzuri ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, haya anayafanya kwa kuzingatia mahitaji ya pande zote za Muungano; na kwa sababu yeye mwenyewe ni mtu wa haki, Waswahili wanasema, "Haki na usawa vinaposhamiri katika jamii yoyote, undugu hujengeka na maovu hujitenga." Ukiona hilo la maridhiano leo linaloendelea, limetufanya tuwe wamoja na wenzetu wa vyama vingine vya siasa.

Mheshimiwa Spika, na haya anayoyafanya kwa kuzingatia mahitaji ya pande zote za Muungano na kwa sababu yeye mwenyewe ni mtu wa haki, na waswahili wanasema haki na usawa vinaposhamiri katika jamii yoyote undugu hujengeka na maovu hujitenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiona hili la maridhiano leo jinsi linavyoendelea limetufanya tuwe wamoja na wenzetu wa vyama vingine vya siasa. Na hii haishangazi kwa sababu

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni tunda la CCM, chama kinachoamini kwamba, binadamu wote ni sawa, chama kinachotambua kwamba, kila mtu anastahili kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake, chama kinachoamini katika misingi ya ujamaa na utu na ujamaa maana yake ni misingi ya utu, haki na usawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni tuda halisi la CCM. Kwa kweli, ni tunda la Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, ni tunda la hayati Abeid Amani Karume, ni tunda la Mzee Mwinyi, ni tunda la Hayati Benjamin Mkapa, ni tunda la Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, ni tunda la Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, ni tunda la CCM na ni tunda la Tanzania. Hii ni tunu ambayo tunayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunamzungumzia mtu ambaye ameweka bayana kwamba, sauti yake na uwezo aliopewa na Mungu na nafasi aliyopewa ya kuwa Rais wa nchi yetu hapendi kumfokea wala kumkemea mtu, yeye mwenyewe anasema na tunamuona kutoka usoni. Matendo yake, kama ulivyoona juzi akipokea Ripoti ya CAG, katika mambo ya hovyo uliona uso wake; kwa mara ya kwanza ametoa maneno mazito kwa sababu amelazimika, ameona kuna watu hawatembeinae, hawatembei katika mapito ya njia anayoionesha. Wanafisadi uchumi wa nchi hii wakati yeye anahangaika halali kutafuta fedha kwa ajili ya ustawi wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wachache wameamua kutumia fursa walizopewa katika uhujumu wa uchumi wa nchi. Katika jambo hili la msingi mama hakuweza kuficha sura yake ya ndani, ililazimika atoe kauli ambayo inawafanya wale wengine wote ambao wamepewa dhamana na Dkt. Samia Suluhu Hassan wajue kwamba, mama hafanyi masihara katika kuleta ustawi wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na ndio maana natumia nafasi hii kuwataka wale ambao wamepewa dhamana na Dkt. Samia Suluhu Hassan, baada ya tamko lake alipopokea Ripoti ya CAG na Ripoti ya TAKUKURU wachukue hatua kumsaidia Dkt. Samia Suluhu Hassan kutoa adhabu ambayo Watanzania wataiona. Hasira ya Mama Samia haiwezi kwenda bure, Bunge lako Tukufu lazima katika siku zinazokuja kwenye mkutano huu tutoe msimamo ambao utahakikisha kwamba, Hasira ya mama kwa wale waliofisadi uchumi wa nchi hii wanachukuliwa hatua bila kutizama sura zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, muoneeni huruma, amekwenda Marekani amemleta Makamu wa Rais, amekwenda Falme za Kiarabu ameleta maendeleo, amekwenda Ufaransa ameleta maendeleo katika nchi yetu. Leo watu wachache tu waliopewa dhamana wanatumia nafasi hiyo kujineemesha wenyewe halafu bado mpaka leo imeshaisha wiki tangu ripoti imetajwa hatujasikia wakubwa wanachukuliwa hatua; tunataka wachukuliwe hatua, hatuwezi kumuunga mkono Rais kwa maneno, lazima tumuunge mkono Rais kwa vitendo. Na kama hamtachukua hatua tukiwa kwenye Bunge hili tutakuja na hoja nyingine dhidi ya wale ambao wamekabidhiwa dhamana na Rais ya kuwashughulikia hawa ambao bado hawajashughulikiwa. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, Mwalimu Nyerere alisema uhuru bila demokrasia ni udikteta, lakini demokrasia bila nidhamu ni fujo. Uhuru bila demokrasia ni udikteta na ndio maana mama amesema hataki kwamba, uhuru wetu ugeuke kuwa ni udikteta kwa watu wengine, amehakikisha kwamba, haki inashamiri katika nchi, misingi ya utu inasimamiwa, heshima ya mtu inathaminiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tunasema pamoja na uhuru tuliopewa, lakini Mwalimu anasema uhuru bila demokrasia ni udikteta, lakini demokrasia bila ya nidhamu ni fujo; sasa

tutumie nafasi yetu ya uhuru tuliopewa kuhakikisha pia kwamba, hatufanyi fujo kwa kutumia uhuru huo bila mipaka, tujiongoze wenyewe ili tujenge Taifa ambalo lina ustawi, umoja na mshikamano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naona umekaa mkao wa kuniashiria, lakini nitoe rai tu kwetu Watanzania wote na vyama ambavyo tunavyo vya siasa; kwanza nawapongeza viongozi wa vyama vya upinzani kwa kuendelea kufanya maridhiano na Rais wetu, kwa kutanguliza maslahi ya Tanzania mbele. Sasa tumeanza vizuri, tumalize vizuri, tusiachane njiani, hii nchi inahitaji umoja na kila mtu na kila mmoja aweke tofali, nchi hii iendelee kusonga.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ninaunga mkono hoja hii. Na Mungu aibariki Tanzania, Mungu ambariki Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsanteni sana. Waheshimiwa Wabunge nina changamoto kubwa moja leo ambayo pengine haijawahi kunipata huko kabla. Kwa sababu tuko kwenye Azimio hili la Kumpongeza Mheshimiwa Rais, halafu mtu akiwa anatema ile mistari kumkatisha, nimeshasema ni dakika tano, inakuwa kidoko changamoto. Kwa hivyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge, ili wale ambao wameomba fursa ya kuchangia na wao wapate, kila mmoja atumie muda aliopewa wa dakika tano tafadhali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mbarouk Nassor Mbarouk, atafuatiwa na Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji. Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa hii fursa na mimi niweze kuchangia kidogo

katika hii hoja. Sisi kwa Wizara ya Mambo ya Nje, jukumu letu moja kubwa ni kuhakikisha kwamba, diplomasia ya uchumi inaendelezwa kwa nguvu zote, lakini nashukuru kwamba, kazi hii sasa imekuwa rahisi kwa sababu, hapo kabla kidogo tulikuwa tunasuasua, lakini sasa kwa kweli tunafanya kazi vizuri sana na hii yote ni kutokana na Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kusafisha njia na huko tunakopita sasahivi tunapita vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nifahamishe kwamba, hivi sasa katika balozi zetu kuna msururu mkubwa sana wa wawekezaji ambao wanataka kuja kuwekeza nchini Tanzania. *List* ni kubwa sana na tunafanya kila juhudi kuhakikisha kwamba, wawekezaji hawa wanakuja Tanzania na kuchangia uchumi wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine, katika kipindi hiki tumeshuhudia biashara na nchi jirani imeongezeka sana mpaka kufikia kipindi kwamba, wengine wanalalamika, mbona bidhaa nyingi zaidi zinakuja kutoka Tanzania kuliko sisi tunavyopeleka Tanzania? Na hizi zote ni juhudu za Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, na suala jingine ni kwamba, hizi ziara ambazo Mheshimiwa Rais anafanya tayari zimeanza kuleta matunda na zimekuwa zikizidisha ufanisi wa Wizara yetu. Kwanza, nitataja mfano mmoja tu; ziara yam waka jana ya Mheshimiwa Rais ambayo aliifanya China, makubaliano 15 ya ushirikiano walikubaliana na tayari utekelezaji wa makubaliano hayo umeshaanza na hasa ikiwemo upelekaji wa bidhaa nyingi kwenda nchini China. Hizi zote ni fursa ambazo nchi yetu inatakiwa izitumie kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, na kwa kumalizia niingine sasa kidogo katika maridhiano ya kisiasa; hili pia limeturahisishia sana kwa sababu, wenzetu wanapokuja katika Wizara zetu

suala hili kila siku lilikuwa ndio gumzo, lakini hivi sasa hawalisemi tena kwa sababu, wanaona kwamba, siasa zetu zimekuwa ni za kirafiki, za kindugu, sio tena siasa za ugomvi na sio tena siasa za chuki. Na hii yote inasaidia katika kupaisha diplomasia ya uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka. Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo ajiandae.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya upendeleo, ili niwe ni miongoni mwa Wabunge ambao wamechukua nafasi hii kuunga mkono azimio hili la kumpongeza mama yetu. Sasa naomba nisema hivi, na nitazungumza kwa ufupi, ili na wengine wapate nafasi.

Mheshimiwa Spika, naomba kwanza kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu. Tumshukuru kwa sababu, kwanza ameamua kutekeleza kwa vitendo kulinda na kuheshimu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwenye hili, waswahili wanasema mnyonge mnyongeni, lakini haki yake mpeni; kwa kitendo chake cha kushirikisha vyama na wadau mbalimbali, ili kuhakikisha kwamba, nchi yetu inaendelea kuwa na amani na yenye maendeleo, tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa maana hiyo kwenye mfumo huu wa demokrasia kuna msemo wa Kiswahili unasema, wengi wape lakini wachache wasikilizwe. Kwenye hili, mama yetu ameonesha mfano kwa vitendo na sisi kama Wabunge, kama Bunge, tunao wajibu wa kuendelea kumuunga mkono kwa sababu ni jambo alilolifanya kwa vitendo kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini naomba niendelee kusema hivi kwamba, kwenye hoja ya mambo ya uchumi mama yetu amefanya mambo mengi. Wenzangu wamezungumza mambo mengi sana, ametoka nje, ametafuta wawekezaji, Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumza pale wawekezaji wengi wako njiani wanataka kuja, sisi naomba Waheshimiwa Wabunge tumuunge mkono mama yetu. Tumuunge mkono kwa sababu, jitihada hizi zinahitaji amani, jitihada hizi zinahitaji imani, bila ya imani wawekezaji hawawezi kuja, lakini bila ya amani wawekezaji pia hawawezi kuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kule nyuma niliwahi kusema kwamba, amani tuliyonayo Tanzania ni tunda adimu ambalo duniani halipo, tuendeleze. Na sisi Wabunge tukishikamana tunaweza kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ningeomba basi kwa sababu, jitihada zote zinazofanyika ni kuweka nchi pamoja, ni kuweka wananchi pamoja, ili tuweze kujenga Taifa letu, ningewaomba sana basi tumuunge mkono katika jitihada zake za kuhakikisha kwamba, uchumi unaendelea kukua. Mama yetu naomba tukuthibitishie uchumi huu utakua, lakini na wewe mama yetu endelea kutupa nguvu, ili tukupe nguvu, ili kazi ziende vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hili kwa sababu hii, Mheshimiwa Ole-Sendeka amezungumza hapa kwamba, kwa kweli mama yetu anafanya jitihada za kuleta

wawekezaji, lakini tuko baadhi yetu ambao tunamshika mashati, ili kumrudisha nyuma. Kule nyuma mama aliwahi kusema, rangi zake ni nyingi tusizitafute, lakini juzi tumeiona moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niombe hivi, na ninaomba niombe kwa heshima kubwa sana, mama amezungumza lugha nyepesi ya kistaarabu wale wenyewe wajitathmini na watupishe. Sikuelewa hiyo lugha yake, lakini naomba niiseme hivi, wale waliopewa nafasi na wanazijua nafasi zao kwamba, mama amechukia kwa sababu tunamrudisha nyuma, naomba sana tumpishe ili afanye kazi zake, tusimrudishe nyuma. Na mama yetu tunakuomba sana, umewapa nafasi na waswahili wanasema mwenye kuvuliwa nguo huchutama, naombeni sana wale wote wenye kujijua hili wasisubiri kuvuliwa nguo halafu tukawazomea maana kwa kweli, tutawazomea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kwa heshima na taadhima Waheshimiwa Wabunge tuunge mkono jitihada hizi, mama amefanya kazi kubwa, anaendelea kufanya, lengo na dhamira yake ni kuhakikisha kwamba, Taifa letu linasonga mbele, naomba sana. Kwenye hili naomba nitoe angalizo au nitoe pendekezo; mnaposafiri baharini wako wengine wanayo kawaida ya kutoa boti, sasa ili boti hili lisizame naomba tukubaliane hivi, wale ambao tunawaona wanaendelea na wana jitihada za kutoa boti, ili tusifike safari yetu, tunaomba tuwatose kabla hatujazama sote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba ajiandae.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kunipa nafasi niweze kuchangia Azimio hili la Bunge. Nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuwa miongoni mwa Marais wachache sana hapa duniani wanaoheshimu Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Katiba ya nchi yoyote ile huwa inakuwa na mapungufu yake. Na katika mapungufu hayo kwa kwaida wengi wa viongozi huwa wanaziogopa Katiba zao, lakini mama ameweza kuwa shujaa wa sasa kuruhusu hata mikutano ya vyama vingi, sio kitu rahisi kabisa, kukaa kiti kimoja na mtu ambaye ni hasimu wako huwa ni kitu kigumu sana. Tunaona hata katika michezo Yanga na Simba tu ni michezo ya kawaida, lakini watu wanavyoweza kupigana vijembe, sasa katika hilo nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuheshimu Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Katiba yetu iko wazi, inasema nchi hii ni ya vyama vingi kwa hiyo, kwenda kinyume cha hapo ni kwamba, mtu anakuwa haheshimu Katiba. Kwa hiyo, namshukuru na ninampongeza sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, lakini nchi hii imeingia kwenye mikataba mingi ya haki za binadamu, ikiwemo ile ya *human rights* ya mwaka 1984 ambayo Tanzania tulisaini mkataba ule. Sasa kwenda kinyume na mikataba ile tunakuwa hatutendi haki kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais, lakini Mheshimiwa Rais amekuwa kimataifa sasa anajulikana kila pembe kwa namna anavyofanya kazi yake katika kuhakikisha sisi sasa tunajikomboa kiuchumi na tunasonga mbele.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni unakumbuka Mheshimiwa Rais alipata tuzo ambayo ilitolewa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu, tuzo ile inaitwa *BABAKAR NDIAYE AWARD.* Alipata ile tuzo kwa sababu, ya ule mchango wake unajulikana sasa kimataifa jinsi anavyofufua uchumi wa nchi yetu kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini lingine, hivi juzi tu tulikuwa kwenye Kamati ya *PAC,* tumezunguka sehemu nyingi

tumeona miradi mingi ambayo sasa inaendeshwa ten ana wenzetu wawekezaji kutoka nje wengi sana sasa wanakuja Tanzania kwa sababu, sasa Mheshimiwa Rais ameifungua nchi na kila siku tunaona vikwazo vinaendelea kuondolewa kwa ajili ya wawekezaji kutoka nje. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini na wengine wamesema hapa, Mheshimiwa Rais juzijuzi hapa alikuwa ametuletea ugeni mkubwa sana wa Makamu wa Rais wa Marekani. Nchi ya marekeni kupata ugeni mkubwa kama ule, yeye Mheshimiwa Makamu wa Rais kufika tu hapa Tanzania, ujio wake sisi Tanzania tumejulikana dunia nzima kwa sababu, Marekani kiongozi wake anapokwenda mahali popote duniani ni karibu dunia nzima inafuatilia kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa ujio wa Makamu wa Rais wa Marekani.

Mheshimiwa Spika, lakini pia na yale ambayo wameweza kuzungumza kuhusiana na mambo ya kiuchumi na namna ambavyo Marekani wanaweza kusaidia katika kuendeleza uchumi wa nchi yetu, tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nimalizie kwa kusema Katiba, ambayo nimesema Mheshimiwa Rais anaiheshimu sana, nchi nyingi hata ambazo zimekuwa zikisifiwa kwamba, zina Katiba nzuri tumeona hata majirani zetu fulani hapa, siwezi kuwataja jina lao, siwezi kutaja hiyo nchi, pamoja na kusifu kwamba, Katiba yao ni nzuri, watu wanaendelea na maandamano. Kwa hiyo, narudia kusema Mheshimiwa Rais kuruhusu maridhiano ya kisiasa hapa Tanzania ule ni ushujaa mkubwa sana kauonesha na sisi tutamuunga mkono, kilichobaki sasa hivi tuendelee kushindana kwa hoja, tuende tuwapalekee wananchi nini kimefanyika katika awamu zetu zote katika utawala wetu wa Tanzania. Tukashindane kwa hoja milango

kwa kuwa iko wazi sasa hakuna vile visingizio vya kwenda kutukanana hadharani.

Tuendelee kushindana kwa hoja, twende tuwapelekee wananchi nini kimefanyika katika awamu zetu zote katika utawala wetu wa Tanzania. Tukashindane kwa hoja, milango kwa kuwa iko wazi sasa hakuna vile visingizio vya kwenda kutukanana hadharani.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba na mimi naunga mkono hoja azimio hili kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, atafuatiwa na Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba ajiandae.

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Mheshimiwa Spika na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi na nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa Mbunge wa Biharamulo Magharibi kwa kuleta hoja hii. Mambo matatu tu katika kuunga mkono hoja hii. Jambo la kwanza ni kihistoria kidogo.

Mheshimiwa Spika, siku ya tarehe 4 Julai, 2001, nchi yetu ilikumbwa na msiba mkubwa. Tuliondokewa na Makamu wa Rais Mheshimiwa Dkt. Omar Ali Juma; na Mheshimiwa Benjamini William Mkapa, Mungu amrehemu, wakati analihutubia Taifa alitumia nafasi hiyo kwa kutumia maisha ya Dkt. Omar Ali Juma kutoa mafunzo ambayo tumeyapata. Kwamba tuna mafunzo sita kuhusu sifa za msingi ambazo kiongozi wa kitaifa Tanzania anapaswa kuwa nazo, alitoa sifa sita. Na mimi miaka miwili ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ninaridhika kwamba hizi sifa ambazo Mheshimiwa Benjamini William Mkapa alizitoa tarehe 4 Julai, 2001

Mheshimiwa Rais anazo; na kwa ridhaa yako naomba nizitaje.

Mheshimiwa Spika, sifa ya kwanza ni utu na uadilifu, sifa ya pili aliitaja upendo na heshima kwa watu wote, sifa ya tatu kupenda kazi na kutumikia wananchi badala ya kupenda kutumikiwa na kutukuzwa, sifa ya nne aliitaja kuweka mbele maslahi ya Taifa na Watanzania badala ya maslahi binafsi au ya kikundi, sifa ya tano unyenyekevu badala ya kupenda makuu na sifa ya sita, na kwa maoni yangu ni muhimu sana, kuzingatia kikamilifu misingi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, na aliitaja misingi hii tisa ambayo kwa hakika Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan anaizingatia kikamilifu. Msingi wa kwanza wa Taifa utu, pili haki, tatu usawa, nne fursa sawa, tano amani, sita umoja, saba upendo, nane mshikamano na ya mwisho namba tisa ambayo ni muhimu sana Muungano wetu wa Tanzania Bara na Zanzibar. Hakuna shaka katika miaka yetu yote katika nchi hii Muungano wetu upo salama sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili,hakuna shaka kwamba mambo haya yote Mheshimiwa Rais anayafanya kwa utashi kwa ujasiri na kwa kuzingiatia katiba na Sheria za nchi yetu. Lakini kumekuwepo na jitihada za hapa na pale kwa baadhi ya watu kujaribu kumtenganisha Rais wetu na Chama cha Mapinduzi. Nataka nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu anayoyafanya haya yote ili kutekeleza kikamilifu Ilani ya CCM.

Mheshimiwa Spika, na nitoe mfano, katika Ilani yetu *paragraph*118 ukurasa wa 166 tumesema hivi; katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama cha Mapinduzi kitaendelea, sikiliza hiyo, kuheshimu na kulinda misingi ya demokrasia na haki za binadamu kwa ajili ya ustawi wa Taifa hili. Kwa hiyo

suala hili Mheshimiwa analifanya kwa kutekeleza Ilani ya CCM kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, lakini *paragraph* ya 250 ukurasa wa 298 ameweka wazi. Ilani inasema katika kipindi cha miaka mitano ijayo Chama cha Mapinduzi kitaendelea kutekeleza jukumu la kihistoria la kimapinduzi la kuongoza pambano la kutetea na kulinda utu, usawa na haki chini ya misingi ya Ujamaa na Kujitegemea. Katika kutimiza wajibu huu CCM itaendelea kusimamia mambo matano yafuatayo, jambo la nne ni kuimarisha demokrasia nchini. Kwa hiyo wale wanaodhani kwamba wanajaribu kumtenga Rais na CCM wamenoa ni sehemu Rais anatekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho; baada ya kupokea *report* ya *CAG* juzi, Mheshimiwa Rais ameshatekeleza jukumu lake, yamebaki majukumu mawili. Jukumu la kwanza kwa Bunge hili na jukumu la pili ni kwa Serikali kupitia Mawaziri wetu. Mimi niwaombe katika muda tulionao siku 88 za kukaa hapa Bungeni tunatarajia kuona kutoka Serikalini majibu yatakayo jibu zile changamoto za kimfumo, kisheria na kikanuni; tuzione kutoka kwa Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wetu Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Rais kaongea kwa uchungu sana kama alivyotoka kusema Mheshimiwa Ole-Sendeka kazi yetu; hiyo ni kazi ya Serikali, kwa upande wetu sisi. Sisi Tanzania hatuna utamaduni wa kupisha. Kazi yetu Wabunge tuwaoneshe wenzetu, ambao Mheshimiwa Rais amewasema, mlango wa kutokea. Kazi hiyo duniani huwa haifanywi na Serikali, huwa inafanywa na Bunge. Tunatarajia Bunge hili, watu wote ambao Mheshimiwa Rais amesema wapishe hawajaona mlango sisi tuwaoneshe mlango. Katka miezi hii mitatu hilo ni jukumu la msingi la Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika,baada ya kusema hayo na mimi nichukue nafasi hii kwa heshima kubwa ninaunga mkono hoja hii tuendelee kumuunga mkono Mheshimiwa Rais na Rais popote alipo atembee kifua mbele ajue Bunge hili linamuunga mkono, lipo naye usiku na mchana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Aida Joseph Khenani atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mheshimiwa Riziki ajiandae.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii na mimi niungane na Bunge lako Tukufu kumpongeza Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo anaendelea kusimamia na kutekeleza majukumu yake kwenye Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nimepata nguvu ya kusimama kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa mambo kadhaa. Jambo la kwanza ni namna ambavyo alipokea Taifa hili kwenye mazingira magumu mpaka hapa alipotufikisha, halikuwa jambo rahisi. Lakini pia kuiaminisha jamii kwamba kiongozi sio mwanaume peke yake na mwanamke anaweza kufanya na akafanya vizuri. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mazingira hayo ameonesha kama kiongozi lakini ameonesha njia. Kwa sisi ambao tuko hapa kwenye chombo hiki kwa niaba ya Watanzania, kwamba matamanio yake ili ayafikie lazima Bunge tutimize wajibu wetu wa kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Spika, natambua mengi yamezungumzwa na Wabunge wenzangu kuhusu kukuza demokrasia; lakini napata mazingira magumu sana, kwamba ni kweli amekuza demokrasia lakini amekuza demokrasia iliyodondoshwa na nani? Wa chama gani? Hayo maswali lazima tujue kwamba

na jamii inayotusikiliza inapata maswali hayo hayo. Tunapozungumzia mikutano ya hadhara; yalizungumzwa hapa tena na kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu kwamba lazima tutenge muda wa kufanya kazi na muda wa mikutano na tulipiga makofi Wabunge ndani ya Bunge hili. Leo tunapongeza kurudisha mikutano ya hadhara ni kweli. Tunampongeza amerudisha lakini nani aliiondoa? wa chama gani? Sisi Bunge tunasimama wapi?

Mheshimiwa Spika, nipongeze…

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa kuna taarifa, iko wapi? Mheshimiwa Cosato Chumi.

**T A A R I F A**

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Naomba nimpe taarifa msemaji anayezungumza hivi sasa. Wakati Mheshimiwa Boutros Boutros Ghali alipogombea nafasi ya *UN* aliomba kwamba yeye atagombea kwa kipindi kimoja, ilipokuja mara ya pili akasema anabadilisha atagombea tena mara ya pili. Akaulizwa kwa nini? Akasema ni mjinga tu asiyebadilisha mawazo yake na kuendana na hali na nyakati. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nimwambie Mheshimiwa Chumi kaka yangu nimepokea taarifa sasa sijajua nani ni wajinga ambao wameamua kubadilisha utaratibu waliokuwanao na kuja na utaratibu mwingine.

Mheshimiwa Spika, maridhiano yanayoendelea ni maridhiano ambayo yana afya kwa Taifa. Ili ufikie uchumi tunaoufikiria ni lazima uruhusu mawazo mbadala. Mawazo mbadala utayapima kama yana maslahi kwa Taifa utayatumia kwa sababu Taifa ni la kwetu sisi sote.

Mheshimiwa Spika, naunga sana mkono azimio hili kama sisi tutaendelea kumsaidia. Ukimtazama mazungumzo yake anatamani kulitoa Taifa lilipo na kulipeleka mahala fulani; lakini tukikaa kwenye unafiki hatutamsaidia Mheshimiwa Rais. Tukisimama imara kumpongeza, leo tukitazama uchumi wa watu pamoja na vitu, Bunge tukisimama imara tutamsaidia Mheshimiwa Rais na tutampongeza kwa sifa anazostahili kusifia. Tutampongeza Mheshimiwa kwa kuimarisha uchumi kwa kusimamia vyema kama Bunge kuondoa mianya yote ya Rushwa na matumizi mabovu ya fedha.

Mheshimiwa Spika, yote haya ambayo ameyaanzisha Rais wetu jambo jema la kupongezwa lazima liwekwe kwenye msingi bora wa Sheria Mama ambayo ni Katiba mpya. Katiba iliyopo si kwamba yote ni mbovu lazima maboresha yafanyike. Maboresho ya kwanza ni kuanzia kwenye Sheria yenyewe ya Uchaguzi, namna tunavyopatikana na namna ambavyo tunaweza kupata viongozi wengine kutokana na wananchi wenyewe walivyoamua.

Mheshimiwa Spika, ili tufikie malengo ya hayo maridhiano ambayo leo Mheshimiwa Rais ameongoza majadiliano hayo ni lazima, tunapozungumzia Sheria hii ambayo ni Katiba mpya, ameonyesha kwamba Chama Cha Mapinduzi mko tayari; ni lazima mchakato huo uanze mara moja ili kusimamia yale anayoyazungumza. Atapokuja Rais mwingine afuate misingi ya Sheria yetu ambayo ni Katiba mpya ya nchi yetu. Tusipofanya hivyo, leo Rais tunampongeza hapa akija Rais mwingine atakuja na nini?

Atakubali hiyo mikutano ya hadhara? Au ataiondoa tena wakati iko kwa mjibu wa Sheria kwenye Katiba yetu ya nchi? Ni lazima misingi inayowekwa leo kwenye utawala bora ije isimamiwe na yeyote atakayepata nafasi hiyo.

Mheshimiwa Spika, si kwamba tunapozungumza kama vyama vya Serikali mbadala tunazungumza mabaya tu. Tumeanza kuonesha njia kabla ya leo, tarehe 8 Machi Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kupitia Baraza la Wanawake (BAWACHA) walimkabidhi tuzo ya kuimarisha demokrasia. Kwa hiyo, sio jambo baya, ni jambo jema, mnapoona jambo linafanyika lazima tupongeze, lakini tupongeze tukiamini haya mambo yamejengwa kwenye msingi imara. Katiba mpya ni sasa Katiba mpya ni lazima. Ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nikawa najiuliza hapa maswali mengi Mheshimiwa Aida unasema tutampongeza. Kwa hiyo, katika miaka yake hii miwili bado hujaona cha Kupongeza. Maana naona unasema tutampongeza, tutampongeza. Tunampongeza sasa kwa aliyofanya baadae tutampongeza tena upya; kwa hiyo anza na hili ambalo limeshafanyika kwa sasa, ukianza tutampongeza maana yake kama tumejiegesha hivi tunamsubiria. Inabidi tumpongeze kwa pale alipofikia tunarudi huku pale alipoanzia na mpaka hapa alipofika ndio msingi wa pongezi za leo. Alipotoka mpaka hapa kule mbele tusubiri na kwenyewe tutakutazama kwa namna inavyokuja si ndivyo jamani?

Mheshimiwa Dkt.r Mwigulu Lameck Nchemba atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mheshimiwa Bahati Keneth Nollo ajiandae.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ili na mimi niweze

kuchangia azimio hili, na kabla sijaongea niseme moja kwa moja kwamba naunga mkono azimio hili. Ni azimio ambalo limekuja kwa wakati na ni azimio ambalo limebeba uhalisia.

Mheshimiwa Spika, sisi kwa upande wa Wizara ya Fedha tunavitu vingi vya kusema ambavyo vimeshajitokeza katika kipindi cha miaka miwili ambavyo vina beba uzito wa azimio hili. Hivi tunavyoongea katika bajeti hii tunayoitekeleza kwa jitihada za Mheshimiwa Rais za kukuza Demokrasia pamoja na Diplomasia ya Uchumi Kwenye bajeti yetu tulipata dola 500, sawa na trilioni 1.2 katika mwaka wa fedha huu ambao tunaendelea kutekeleza; na hii ni kupitia dirisha la *Development Policy Operation, DPO* ambayo inatolewa na *World Bank*. Dirisha hili lilikuwa limefungwa kwa miaka Takribani saba, Tanzania ilikuwa imetolewa katika dirisha hili kwa sababu vigezo vyake vinapatikana kwa *good governance*, *transparency* na kwa juhudi za kupambana na masuala ya rushwa. Sasa hivi tuko kwenye *programme* hiyo ambayo jumla yake ni dola bilioni moja. Milioni 500 zimeingia katika mwaka huu wa fedha na milioni 500 zinaingia katika mwaka wa fedha unaokuja. Kwa hiyo hii ni jambo ambalo tayari limeshafanyika na dirisha ambalo lilikuwa limefungwa.

Mheshimiwa Spika, lakini sio hilo tu tuko kwenye *programme* mbili na *IMF*, mojawapo tulifanya ile ya *RCF* lakini ya pili tumefanya ile ya *ECF* ambayo ni takribani dola bilioni 1.1. Kwa mwaka wa fedha huu tayari tumeshapata dola milioni 152 *quarter* ya kwanza na *quarter* hii kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha tunaoendelea nao tutapata dola milioni 152 nyingine. Fedha hizi ni za *recovery programme* ndizo ambazo zinaenda kwenye kilimo, umwagiliaji, *modernization* kwenye mifugo na kwenye uvuvi, hili ni jambo ambalo limeshafanyika na ni *programme* ya takribani miezi 40. Kwa hiyo tutaendelea na *programme* hii ambayo ni ya *recovery* na zinakwenda kwenye sekta za uzalishaji. Na hii inapewa nchi ambayo inakidhi vigezo. Na vigezo vyenyewe

vinahusiana na *good governance* pamoja na matumizi bora ya rasilimali.

Mheshimiwa Spika, kuna hatua zingine ambazo ni kubwa ambazo tunaziendea ambazo mataifa makubwa yamefanya. Moja, tuko kwenye hatua za mwisho za *credit rating*, tumeshaonana na magwiji wa kufanya *credit rating* kwenye mataifa, walikuja *Mood's* na wengine tumemaliza nao wiki iliyopita. C*redit rating* inafanyika kwa Taifa ambalo linakidhi vigezo na vigezo vyenyewe ni vya demokrasia pamoja na *good governance*, na diplomasia ya kiuchumi ambayo hiyo Mheshimiwa Rais amefanya na kwenye ukanda wetu huu Tanzania ndiyo ilikuwa na *score* kubwa.

Mheshimiwa Spika, tunatarajia watakapotoa *report* tutakuwa tumepanda juu zaidi, na hii inafanyika na tayari tumeshamaliza tunajua tu *report* itatoka hivi karibuni. Lakini si hilo tuna lingine ambalo tuko hatua za mwisho ni kuweza kupata fedha za *Climate Change RST*. Si hilo tu tunatarajia tupate *accreditation* ya *institution* zetu. Hivi tunavyoenda *accreditation* ilikuwa kwenye baadhi ya sekta binafsi lakini sasa hivi tuko hatua za mwisho ili ofisi ya Rais *TAMISEMI* ipate *accreditation* na Wizara ya Fedha ipate *accreditation,*tutaweza kupata fedha ambazo zinatumika katika kupambana na mabadiliko ya tabia ya nchi na kuweka ustahimilivu wa uchumi pamoja na kuweka sawa kwenye masuala ya *balance of payment*.

Mheshimiwa Spika, lakini si hivyo tu tuko kwenye hatua za mwisho pia kuangalia na kukamilisha urejeshwaji wa *MCC*. *MCC* na yenyewe ilikuwa *programme* ambayo ilikuwa inatekelezwa na imesaidia sana katika kutekeleza miradi ya maendeleo. Tuko hatua za mwisho naamini walivyotoa *report* iliyopita walitumia vigezo vya zamani, tunaamini sasa hivi wakirejea hivyo vigezo ambavyo tunaamini kila mwaka wanakuwa wanatoa hivyo vigezo, tunaamini Tanzania

itakuwa imeshafuzu, na hii ni kwa sababu ya hatua kubwa ambazo zimeshafanyika. Vigezo vyenyewe ni vya mikutano ya hadhara ilisharuhusiwa, masuala ya uhuru wa habari ilisharuhusiwa, masuala ya *data protection* ilisharuhusiwa, *protection of investment* tulishafanya hivyo vitu.

Mheshimiwa Spika, sio hayo tu ni pamoja na masuala ya kupambana na matumizi bora ya rasilimali. Kuweka misingi bora ya matumizi ya rasilimali. Mheshimiwa Rais amepiga hatua kubwa, Mwaka jana tumeongeza fedha kwa *CAG* tumeongeza afanye *late time audit*. Tumeweka fedha kwa Mkaguzi Mkuu wa Ndani. Haya yote ambayo mnaweza mkaona ni kwa sababu ya Mheshimiwa Rais kuweka meno kwa *CAG* lakini pia na kuweka rasilimali kwa ajili ya ufatiliaji na ukaguzi ambao ndio unatoa majibu na kuweza kusaidia Bunge. Kwa hiyo, haya yote yanayofanywa yanaweka uzito kwamba tunatakiwa tumpongeze Mheshimiwa Rais, tumuunge mkono na kila mtu atimize wajibu wake. Sasa dada yangu, namshukuru Mheshimiwa Chumi amemjibu vizuri alipokuwa anasema kwamba watu wanauliza hii ilifikaje ilifikaje, hayo maswali ni ya kila mtu.

Mheshimiwa Spika, tumefika hapa baada ya Mheshimiwa Rais kwenda kwenye maridhiano na akaweka *4R* hizo zote ni za kuweka misingi ya *platform* kwenye uwanja. Uwanja ukiwa *rough* lazima *opponents* awe *tough,* wewe unategemea watu wawe *rough rough* halafu umepewa jukumu la nchi uachie? Hamna nchi inayoweza ikaenda hivyo. Kwa hiyo, kwa kuwa Mheshimiwa Rais amekaa na pande zote, tukakubaliana tuendeshe vipi mambo ya nchi hii, hicho ndicho ambacho na CCM inaunga mkono kwa sababu CCM ndio kiongozi wa ustaarabu wa kuendesha nchi hii, ndio maana tangu uhuru mpaka sasa nchi hii haijawahi kupata dosari yoyote ya kukiuka masuala ya haki za binadamu wala hata yale ambayo yanasimuliwa kwenye hizo nchi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumuunge mkono Mheshimiwa Rais na ameongea vizuri nadhani Mheshimiwa Ole-sendeka ama Mheshimiwa Mwakasaka kwamba haya tunayoyaweka na haya ambayo tunayokubaliana tuyaheshimu na twende nayo na hiyo ndiyo itakayokuwa dira na hiyo ndiyo itakayotupa *sustainability.* Maana yake aliuza kwamba kwa hiyo sasa baadaye itakuwaje? Baadaye itakuwa hivi hivi, tuyaheshimu tu haya ambayo tunakubaliana. Hiyo ndiyo misingi ya demokrasia na hiyo ndiyo misingi ya utawala bora na hiyo ndiyo misingi bora ya uendeshaji wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo tukishaweka mifumo ikafanya kazi tutakuwa tumejihakikishia masuala ya uendeshaji wa nchi yetu na hivi tuko kwenye utengenezaji wa dira mpya na nawahakikishia kwa haya ambayo Mheshimiwa Rais anayajengea sasa hivi, tuna uhakika dira mpya itakapopinduka kwamba tumeshamaliza miaka mingine hiyo ambayo itakuwa ya utekelezaji wa dira, nchi yetu itakuwa imekwishaenda kwenye nchi zilizoendelea na Watanzania watapata manufaa makubwa ya kubadilisha maisha yao na haya ni mambo ambayo Mheshimiwa Rais anayapigania.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze *Engineer* Chilewesa aliyeleta Azimio hili na Mheshimiwa Mbunge tunaliunga mkono mia kwa mia na tunamtakia kila la heri Mheshimiwa Rais katika kuendeleza haya mambo mazuri. Mengine tutaendelea kuyasema katika bajeti za kisekta na mengine tutayasema katika Bajeti Kuu ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Riziki Lulida atafuatiwa na Mheshimiwa Kenneth Nollo, Mheshimiwa Saashisha Mafuwe ajiandae.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuunga mkono hoja ya kuumunga mkono Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli sina la kusema zaidi ya kusema Mwenyezi Mungu ni mkubwa. Mheshimiwa Rais ameonesha upendo mkubwa kwa watu wenye ulemavu. Hata hivyo, kitendo cha kuonesha upendo kwa watu wenye ulemavu, leo dunia inaitambua Tanzania iko katika ramani ya upendo kwa watu wenye ulemavu na walemavu sasa hivi wanasikika na wanaeleweka.

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia maeneo ambayo Mheshimiwa Rais ameonesha. Alikula chakula na watu wenye ulemavu Ikulu na aliwapongeza kwa kazi kubwa waliyoifanya kwa kupigania Mchezo wa Mpira. Akiwakilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwanza alituletea Shilingi Milioni 150 kwa watu wenye ulemavu, wakasema hatutakuangusha, tuliweza kushinda mpira wa *East Africa,* tukashinda Mpira wa Afrika, tukaingia katika *World Cup.* Haya ni mafanikio ambayo hajaweza kufanikiwa Yanga wala Simba. Tunaomba nao wajitahidi kama walivyofanya walemavu. Natamani siku moja nisikie Simba au Yanga wameingia katika mipira mikubwa kama hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia huo mchezo, sasa hivi vijana 12 wameajiriwa nje ya nchi kama ma-*professional Soccer,* wanapata mahitaji yao na wengine wameniambia Mama cha kushukuru hatuna, tunatamani tukirudi kule turudi tena kwa Mheshimiwa Rais kumwambia tumefanikiwa kwa hili na sasa hivi familia zetu zinanufaika kwa ajira zetu nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi sina budi kwa hilo niseme tu Mwenyezi Mungu azidi kumbariki, azidi kuwapenda watu wenye ulemavu na vijana kwa ujumla na watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kupitia Wizara ya Madini, nimpongeze Mheshimiwa Rais mwamko huu na *spirit* aliyokuja nao baadhi ya Mawaziri wanaiga kuonesha *spirit* ya kuwapenda watu wenye ulemavu. Kwa kupitia Shirika la *STAMICO* tumepewa vitalu vya kuchimba dhahabu Mbogwe. Mimi mwenyewe nimekwenda pale kugawa vifaa kwa watu wenye ulemavu wenye usikivu hafifu, leo walemavu wanachimba dhahabu. Je, haya sio mafanikio? Tutanyamaza vipi bila kumpongeza kwa kuona leo walemavu wanataka kuuza dhahabu kwa kujifanya na wao wataondoa umaskini? Naomba na Wizara nyingine na taasisi nyingine ziige kama zilivyofanya Wizara ya Madini na *STAMICO.*

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara ya Kilimo kwa kupitia mfumo huu waliokwenda na wenzao, wao wametoa hekari 50 kwa baadhi ya wilaya kuhakikisha walemavu wenye ulemavu wa ngozi wanaanza kulima. Kwa mfano, Chamwino wametoa hekari 50 kwa watu wenye ulemavu na taasisi ya *ASA* ikishirikisha na mwenyewe Bashe aliwaambia wapeni mbegu, wakapewa mbegu za alizeti na mbegu za mahindi. Huu ni mfano wa kuanza nao kuhakikisha na maeneo mengine wanatoa ardhi kwa watu wenye ulemavu walime. Kwa vile walemavu sio wote ambao hawawezi kulima, walemavu wenye usikivu mdogo wanaweza kulima, walemavu wenye matatizo ya ngozi wanaweza kulima.

Mheshimiwa Spika, sasa hii *speed* ya Mheshimiwa Rais twende nayo vizuri ili angalau tunachosema sasa hivi kuwa haki ya walemavu katika maendeleo *inclusion* yanakwenda sambamba na *speed* ya Mheshimiwa Rais. Mwenyezi Mungu amzidishie zaidi Mheshimiwa Rais na walemavu wanasema wana neno lao kuwa wao wako pamoja na yeye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *CRDB Bank* ikishirikiana na waendesha bajaji 500 wa Jiji la Dar es Salaam, wameamua kwa pamoja kushirikiana nao kwa kufungua akaunti ili walemavu wale wasinyanyasike. Wanachukua mikopo huku mitaani ya shilingi milioni 14 kwa wahuni huko mitaani matokeo yake wanashindwa kurudisha pesa, wanakuwa wanatumika visivyo. Hata hivyo *CRDB Bank* kwa kumuunga mkono Mheshimiwa Rais, kwa kweli ni lazima tuyapongeze haya mashirika ambayo yako karibu na watu wenye ulemavu na tayari tunaona kabisa kama watu wale watawakomboa walemavu ambao wanahitaji mahitaji maalum.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze na niwashukuru Waheshimiwa Wabunge, wakafanye kazi ya kupambana kule chini. Hakuna wa kuachwa nyuma *nobody should be left behind there is nothing about us without us.* Walemavu wanahitaji *inclusion* katika kila eneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana, kwa *speed* hii tunayokwenda nayo Mama ameongea neno moja zito kwa Watanzania amesema, tuwe mabalozi twende tukawalinde vijana wetu kule chini, wasiige tabia na utamaduni ambao sio wa kwetu. Kwa vile Tanzania ni Nchi huru ina sheria zake, taratibu zake, Dini zake, lakini vile vile ina mila na desturi. Hivyo wasituletee mila ambazo zitakuja kuwafanya watoto wetu wawe dhaifu kwa ajili ya wanachokitaka wao hapana.

Mheshimiwa Spika, hili neno limewafanya Watanzania wamekosheka, kuwa na faraja kuwa watoto wetu ambao wanataka kuharibiwa kila mmoja akawe balozi katika eneo lake. i Wabunge katika kila…

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Nani ameomba taarifa simuoni.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Spika, mimi hapa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lulida kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Khadija Taya.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Spika, naomba pia nimkumbushe Mheshimiwa Riziki kwamba Mheshimiwa Rais mwaka 2022 ametoa shilingi milioni 60 kwa ajili ya mafuta ya watu wenye Ualbino na hii iko kwenye mchakato wa Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa hiyo, ninachotaka kumkumbusha kwamba Mheshimiwa Rais anafanya mengi sana ambayo tutaweza kila siku kuyasemea na kuyatetea na kuyapigania. Kwa namna hiyo tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Riziki Lulida unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. RIZIKI S LULIDA:** Mheshimiwa Spika, hiyo taarifa ni lazima niipokee, ni taarifa yenye mafanikio na ni kweli wenzetu wenye matatizo yaN wamepewa Mafuta ya Mabilioni. Sasa hivi tunae balozi wetu ambaye ni Mheshimiwa Mwigulu Nchemba amesimama na watu wenye ulemavu kuhakikisha hela zao za mikopo zinapatikana. Vile vile, Mheshimiwa Mwigulu ni balozi wa watu wenye ulemavu napenda awe pamoja na watu wenye ulemavu ili aweze kufanya nao kazi kwa pamoja ili walemavu hao wasihangaike kuombaomba. Hakuna wa kuombaomba kila mmoja atakuwa pamoja na sisi, tufanye kazi kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema tena naunga mkono hoja hii kwa kusisitiza Mheshimiwa Rais kwa kweli anafanya kazi kubwa kwa kupitia vijana na watu wenye ulemavu. Nasema ahsante na Mungu azidi kumbariki, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kenneth Nollo atafuatiwa na Mheshimiwa Saashisha Mafuwe na Mheshimiwa Tabasamu Hamis Mwagao ajiandae.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika hoja hii ya kihistoria.

Mheshimiwa Spika, kiongozi yeyote duniani hupimwa kwa nyakati na mazingira ambayo anachukua nchi katika kuiongoza. Mazingira aliyoyachukua Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Katika kuiongoza nchi hii, yalikuwa ni mazingira magumu, yalikuwa ni mazingira ya kipindi cha giza, yalikuwa ni mazingira ambayo kila mmoja wetu katika nchi hii alikuwa hajui ni wapi tunaelekea.

Mheshimiwa Spika, katika historia ya nchi yetu hajawahi kutokea Rais aliyepo madarakani akafariki akiwa madarakani. Vile vile, katika nchi yetu ilikuwa ni wakati mgumu kwamba sasa tunakwenda katika mlengo upi? Mazingira aliyotoka nayo Mwalimu Nyerere wakati anaichukua nchi hii yalikuwa tofauti, Mzee Mwinyi hivyo hivyo, Mzee Mkapa hivyo hivyo, Mzee Kikwete hivyo hivyo, Mzee Magufuli ilikuwa tofauti na Mheshimiwa Samia ikawa tofauti vile vile.

Mheshimiwa Spika, uhodari wa Rais Samia unaonekana katika maeneo haya. Kama nilivyosema alichukua nchi wakati tukiwa katika majonzi, vile vile alichukua na kuongoza nchi hii akitoka katika Chama kikubwa ambacho ilikuwa ni kazi ngumu kukiunganisha. Ninyi mnafahamu duniani kote anapotoka Rais madarakani kunakuwa na mipasuko mikubwa, yanatengenezwa mazimwi kumtisha Rais aliyeko madarakani, zinatengenezwa hoja za kusema wale ni wa kwako na wale sio wa kwako, zinatengenezwa hoja kwamba wale ni bora na wale sio bora. Hata hivyo, vikwazo hivi

Mheshimiwa Samia alivuka ndani ya Chama cha Mapinduzi na Chama hiki imekuwa imara.

Mheshimiwa Spika, hapa leo tunaposema, huwezi ukatanabaisha kwamba wale wa Rais Samia, wale sio wa Rais Samia, wale wa Chama cha Mapinduzi bora, wale sio wa Chama cha Mapinduzi bora, wote sisi tumekuwa chombo kimoja kwa sababu ya uthubutu wa Rais Samia.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo sote tutakubaliana wakati Mheshimiwa Samia anachukua madaraka nchi yetu tulikuwa tumehasimiana sana kisiasa kwa tabia zetu, kwa namna tulivyotoka. Mheshimiwa Samia amechukua uongozi wa nchi hii kukiwa vyama vya siasa vina Wenyeviti wakongwe wamekaa miongo na miongo, wamehasimiana huko nyuma. Hata hivyo hakuangalia historia zote, akasema ni lazima tukae pamoja, ni lazima tuanze mwanzo. Ilikuwa ndiyo Rais Samia kama ni kupoteza alikuwa anapoteza. Maana yake aliamua kwamba pamoja na yote yaliyotokea tunataka sasa nchi yetu tuheshimiane katika demokrasia.

Mheshimiwa Spika, katika jambo hili Mheshimiwa Rais amefanya vizuri sana, amewaunganisha Watanzania wote. Nataka niseme katika jambo la kusamehe ni jambo gumu. Mfano tu mdogo, Mheshimiwa Rais amesamehe mambo mengi na amekubaliana na hoja za wapinzani walizokuwa wanasema. Akiwa kwenye Mkutano wa Chama cha Demokrasia wa Wanawake lugha kubwa aliyoongea ni kwamba tusameheane, lakini wenzetu walisema kuna wenzetu 19 hatuwezi kuwasamehe, tuone namna ya kusameheana ilivyo ngumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kusema wengine walienda gerezani sijui na wengine walifanyaje, Rais akasema yote hayo tusameheane, lakini wale wakasema wenzetu 19 hatuwezi kuwasamehe asilani. Kwa hiyo tunampongeza

Mheshimiwa Rais kwa moyo wa kuthubutu na kwa moyo wa kusamehe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nije kwenye suala la uchumi. Mheshimiwa Rais alichukua nchi hii ikiwa na miradi mikubwa. Kwenye reli sote ni mashahidi na mambo mengine. Hata hivyo, tumeshuhudia namna ambavyo miradi yetu imeendelea hakuna namna ambao ulilala ha hili vile vile tunampongeza Rais wetu kwa maana ametuvusha na nchi yetu imeweza kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika diplomasia, sisi tumekaa vizuri, vita ya Ukraine na Russia ni vita ya nadharia katika diplomasia. Ni nani anataka kuwa mbabe na nani anataka wengine aweze kumfuata. Hata hivyo, sisi hapa tumepita vizuri na tumeshikilia msimamo wetu kwamba Tanzania haifungamani na upande wowote na heshima yetu inaendelea kuwepo na tumeendelea kusonga mbele.

Mheshimiwa Spika, vile vile niseme kwenye suala zima la kujenga taasisi, kilichotokea juzi kwenye ripoti ya *CAG* bado tuna shida ya kujenga uwezo wa kitaasisi. Yale yote ambayo Mheshimiwa Rais amesema tena kwa hasira kubwa ni kwamba wale wote wanaokabidhiwa taasisi za kuiongoza nchi hii ni lazima wawajibike vilivyo na ni lazima wafanye kazi vilivyo. Nakubaliana na Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo kwamba Bunge hili lipewe nafasi lisimuonee mtu, lakini ni lazima tutajane, ni lazima tusemane na kwa mazingira ya Rais wetu alivyo, si lazima mpaka ufikishwe hatua ya kutenguliwa. Wapo watu ambao wamefanya makosa hayo, kwa hiyo kwa heshima ya Rais waweze kujiuzulu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Tabasamu Hamis Mwagao na Mheshimiwa Msukuma ajiandae.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye Azimio hili muhimu sana la kumpongeza Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, wenzangu wamezungumza kwa upana kuhusu faida za kukuza demokrasia nchini, lakini nitajielekeza katika ukuzaji wa demokrasia ya kiuchumi. Hata hivyo kabla sijaenda mbali, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge na Watanzania tumuombee sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Rais anafanya kazi kubwa mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitazungumza hapa kwa mifano tu na mwishoni nitataja kule Hai mambo ambayo tumeyaona. Mheshimiwa Rais miradi yote mikubwa ambayo mtangulizi wake alianza sasa hivi kazi inaendelea. Bwawa la Mwalimu Nyerere, Madaraja, kila shughuli ambayo ilikuwa imeanzishwa inaendelea, Mheshimiwa Rais anafanya kazi vizuri sana. Shirika la Ndege, ndege zimeendelea kununuliwa hakuna kilichosimama. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi hiyo kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumze kidogo kwenye demokrasia. Hili tunaloliona Mheshimiwa Rais anapaswa kupongezwa kwa dhati. Niseme hapa wenzetu wa Upinzani waelewe Mheshimiwa Rais ana dhati ya kweli na wao wapokee dhati hiyo kwa kweli. Sio tunazungumza kwenye *level* ya Taifa tunaridhiana halafu huku chini watu wanaenda kufanya vitu vya tofauti. Tuwe na dhati na tuwe wakweli kutekeleza demokrasia ya kweli. Nalisema hili kwa sababu kuna unafiki ndani yake na fitina ndani yake. Huku

wanazungumza lingine na wakifika huku chini wanazungumza lingine.

Mheshimiwa Spika, natoka Jimbo la Hai, tunafahamu changamoto zinazotokana na tatizo la kutokuwa na demokrasia ya kweli. Kwa hiyo kama kuna watu ambao wana neema na wamefurahi kwa kweli ni watu wanatoka Jimbo la Hai kwa sababu tunafahamu changamoto zinazotokana na matatizo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tunafurahi kule hai miradi kedekede inatekelezwa. Tulikuwa na tatizo la maji, pale Boma Ng'ombe tumeletewa Bilioni 3.3 kazi inaendelea. Miaka mingi tulikuwa hatuna barabara, sasa zinachongwa, vituo vya afya vitano vinajengwa, hospitali ya wilaya tumeletewa pale bilioni 3.1, kazi inaendelea na hivi juzi tumeletewa fedha nyingine za madarasa. Haya yote ni mafanikio ya kazi kubwa anayoifanya Mheshimiwa Rais. Tuna kila sababu ya kulinda kazi hizi kubwa anazozifanya kwa dhati.

Mheshimiwa Spika, niseme maeneo mengi yameguswa. Pale kwetu tulikuwa na kiwanda cha *Machine Tools* Kilimanjaro leo kinafanya kazi, kimekufa kwa miaka kumi na tatu, haya ni mambo makubwa ambayo Mheshimiwa Rais wetu anayafanya. Hata hivyo, niseme wenzangu wamezungumza hapa, Profesa amezungumza akasema wale ambao wanamwangusha Mheshimiwa Rais tuwaonyeshe mlango. Hata hivyo, nachelea kusema tuwaoneshe mlango, kwani hawaoni mlango? Mlango si upo? Kesho ita *press* pale, sema bwana mimi naachia ngazi, nimekuwa kikwazo kwa nchi hii, waingie wengine wala hawahitaji kusubiri.

Mheshimiwa Spika, nawashauri wale walioko Serikalini na ameona Mheshimiwa Rais amezungumza kwa lugha ile, Mama yetu tunaempenda sana na yeye ndiyo mzigo humu

ndani, si aende na kuita Waandishi wa Habari sema nalichota bao na tugawane? Tuachie ngazi waingie wengine wafanye kazi wasimkwaze Mama yetu.

Mheshimiwa Spika, niseme, wewe uturuhusu sasa hili Bunge linalokuja tufanye nao kazi, wale wanaomwangusha Mheshimiwa Rais ili Azimio hili liwe na meno ni lazima wale wanaomvuta nyuma Mheshimiwa Rais tushushughulike nao. Walioko huku ndani na hata walioko kule nje ambao wanafanya kinyume na yale ambayo yako kwenye maridhiano.

Mheshimiwa Spika, nimeeleza hapa hawa walioko hapa ndani wanafanya na sisi tutashugulika nao, lakini pia walioko kule nje, hata wenzetu walioko upinzani wajue tunashughulika nao kwa sababu hatuna mzaha kwenye hili, tunataka maendeleo. Vile vile wachukue mfano mzuri, kama kuna maridhiano ndani ya Serikali waende na maridhiano mazuri kwenye vyama vyao. Huko kwenye vyama vyao pia kwenye upinzani kuna uonevu mkubwa mno. Waende na wao wakatekeleze demokrasia kama hatua ya kumuunga mkono Mheshimiwa Rais. Huwezi kuhubiri leo maridhiano halafu wewe kwenye Chama chako unaumiza watu, unakandamiza watu, wewe ni mfalme, unaishi unavyotaka, hapana. Waheshimu katiba za vyama vyao na waheshimu taratibu walizojiwekea kwenye vyama vyao ili nchi hii iwe na amani pande zote. Watanzania tufurahi kwenye nchi yetu, tuishi kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu na mwisho wa siku tutakuwa sasa tumemuunga mkono Mheshimiwa Rais. Hii ya kusema, tunapiga picha tunaridhiana leo unakwenda unaumiza wengine nyuma si sawa. Kama tunaridhiana, turidhiane kwa dhati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima tuseme jambo moja hapa, haya yote mazuri yanayotokana na Mheshimiwa Rais huwezi kuyatofautisha na Wabunge wa CCM. Haiwezekani,

Wabunge ndio wanaopitisha bajeti hapa, kama kuna mazuri anayoyafanya Mheshimiwa Rais, Wabunge tuko hapo chini yake ndiyo tunanyanyua. Vile vile ilani inayotekelezwa ni dhahiri ni Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo haya yote tunayozungumza hapa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, haya yanatokana na Ilani nzuri ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nachukua fursa hii kuwaomba wananchi huko nje walipo wote, wamuunge mkono Mheshimiwa Rais, waiunge ilani yake, wawaunge mkono Wabunge na Madiwani walioko kule, kwa sababu kwa kipindi kifupi mambo makubwa yamefanyika sana sana. Tunaomba Watanzania tushikamane twende kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, nasisitiza kwa kuhitimisha hoja hii kwamba, wale walioko humu ndani na watumishi wa umma walioko nje, ambao kwa sauti ile ya Mheshimiwa Rais unaona kabisa unahusika, *step down* mapema usisubiri tuanze kukutaja, ondoka kiungwana ajali kwenye siasa ni jambo la kawaida utajirekebisha baadaye. Baada ya hapo niombe viongozi na vyombo vya dola vilivyosikia sauti ya Mheshimiwa Rais, pengine watakosa kuona mlango kama alivyosema Profesa hapa, vyombo vya dola viwasaidie kusukuma kuona mlango ulipo. Watusaidie viongozi wa dola ambao wamepewa mamlaka kuwaonesha hao wabadhirifu, hao wezi mlango uko wapi wa kutoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao atafuatiwa na Mheshimiwa Salome Makamba Mheshimiwa Musukuma ajiandae.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii. Nataka kuwaeleza Watanzania kwamba kazi kubwa aliyoifanya Mheshimiwa Rais Samia anazo sifa zote za kupongezwa kama binadamu. Binadamu katika asili akifanya vizuri akasifiwa basi anamshukuru Mwenyezi Mungu, kwa hiyo kwa hatua hii hatujafanya kosa lolote leo ndani ya Bunge hili kupeleka maono yetu na kuyasema yaliyopo katika vifua vyetu nafsi zetu ziweze kuridhika, kazi alizozifanya Mheshimiwa Rais ni kubwa sana katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi anazozifanya Mheshimiwa Rais za usiku na mchana kwa ajili ya kuja kuhakikisha ustawi wa Taifa hili, Mheshimiwa Rais anajitahidi kuweka hali ya hewa katika nchi hii iwe salama. Pamoja na kuweka hali ya hewa kuwa salama katika nchi hii, yapo pia matatizo makubwa sana ya utawala bora sehemu kubwa sana ya utawala bora, kutumia hii dhana ya utawala bora watu wanapata nafasi kubwa sana ya kumrudisha Mheshimiwa Rais nyuma, katika jambo hili ni kwamba tunatakiwa kuwa makini sana wasaidizi wake hasa Bunge ni wasaidizi namba moja kwa kazi anazozifanya Mheshimiwa Rais katika kumuunga mkono.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya *CAG* imepokelewa na kikanuni inatakiwa ije hapa ndani baada ya siku Saba, haya yote Mheshimiwa Rais aliyoyasema wakati anapokea taarifa ile alikuwa katika saumu, alichukia akiwa amefunga, sasa nasi tunatakiwa tuchukie huku tumefunga tuko ndani ya saumu. Hii siyo dhambi na wala hatutatengua saumu zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bajeti iliyokuwa imepitishwa hapa haikuwa na fungu la wezi, naomba nirudie, tulipitisha bajeti pesa ziende kwenye shughuli za maendeleo hakukuwa na fungu la wezi. Sasa fungu la wezi linatokea kila taarifa ya *CAG. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo Mama amepokea taarifa ya pili ya *CAG* na akaonesha ujasiri kusema hadharani amekerwa na akatumia lugha ambayo siyo ya staha ndani ya mwezi wa Ramadhani. Mimi mwenyewe siku hiyo wakati anatumia ile lugha nilichukia zaidi yake sina nafasi tu, ngoma iletwe Bungeni hapa halafu tuoneshe hali ya hewa kwamba tunamuunga mkono Mheshimiwa Rais kwa dhati, tumechoka na wizi.

Mheshimiwa Spika, tulitegemea kabisa pamoja na mambo mazuri yanayofanyika huko wataalamu wetu wanafanya kazi lakini wako Wataalam ambao siyo wazalendo, wako Viongozi wenzetu ambao siyo wazalendo, taarifa hii kwa sababu haijawa dhahiri lakini tukiipitia ripoti ya *CAG* safari hii tunaomba dakika 20 kuchangia ili tutoe adabu isije ikajirudia tena. Kanuni ziko kwako leo tunamsifia Mheshimiwa Rais tunataka tukusifie na wewe safari hii utuwekee hii taarifa tuinyambue sawasawa, uingie kwenye historia kuzuia wezi katika nchi hii. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Salome Makamba atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, tutamalizia na Mheshimiwa Festo Sanga.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Nami niungane na hoja ya Mheshimiwa Mbunge ya kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuimarisha demokrasia na sera ya mambo ya nje kwa maana ya *foreign policy*.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kwamba nafikiri hatumuelewi vizuri Mheshimiwa Rais ukiniambia niseme kwa

neno moja nitasema Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ni Balozi wa nchi za Afrika. Nitoe mfano mdogo, pamoja na mambo mengi aliyoyafanya, juzi alizungumzia kuhusiana na sheria iliyotungwa huko Marekani inayozipa nchi za Afrika fursa ya kupeleka bidhaa, huduma na utaalam kwenye nchi ya Marekani, hiyo sheria ilipitishwa mwaka 2000 na haijawahi kutekelezwa kwa miaka 23 sasa, lakini juzi Makamu wa Rais wa Marekani alipokuja Tanzania pamoja na kutembelea nchi zote Mheshimiwa Rais aliamua kusimama kwa Afrika, akaomba nchi za Afrika mkataba ule utekelezwe, pamoja na hilo pia aliomba Visa ya Watanzania kwenda Marekani iongezwe muda isiwe na ukomo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana ya Mheshimiwa Rais kuifungua Afrika au kuifungua Tanzania kwenye nchi za ulimwengu wa Kwanza ni kwamba Watanzania tuweze kwenda kupeleka bidhaa zetu kwenye nchi za ulimwengu wa Kwanza ikiwemo Marekani. Tupeleke utaalam wetu, tupeleke Wakandarasi wetu wakafanye kazi kule kama ambayo Wakandarasi na bidhaa za kule zinakuja Afrika.

Mheshimiwa Spika, sasa ili hayo mambo yaweze kutekelezeka kwa vitendo ni lazima tumsaidie Mheshimiwa Rais kuwaandaa watu wetu, kuandaa vyombo vyetu, kuandaa mazao yetu *raw materials* zote ziweze kupelekwa kwenye maeneo hayo. Sasa ili hayo yafanyike ni lazima Bunge na Serikali tushirikiane katika kuhakikisha taratibu, sheria, kanuni, mienendo na mfumo wa nchi unaweza kuwandaa Watanzania kukimbilia fursa hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi tunawezaje kupeleka wataalam wa kitanzania ambao wanaweza kwenda kufanyakazi kwenye nchi za ulimwengu wa kwanza, kama tangu Bunge hili mimi ninakaribia miaka Nane kwenye Bunge hili, tumeomba tubadilishe mitaala ili wanafunzi wetu waweze

kwenda kufanya kazi katika nchi za nje mpaka leo mitaala haijabadilishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliwahi kutoka agizo ndani ya Bunge hili tukufu kwamba vitabu vya kiingereza vyote vibadilishwe viwe vya Kiswahili, agizo hili lilitimizwa ndani ya miezi mitatu tu leo tuna miaka miwili ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mtaala wa Elimu wa Tanzania haujabadilika.

Mheshimiwa Spika, tunawezaje?

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, Taarifa

**SPIKA:** Mheshimiwa Salome Makamba kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Husna Sekiboko.

**T A A R I F A**

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Salome Makamba kwamba agizo la Mheshimiwa Rais la kuboresha mitaala limeshafanyika na hivi juzi Wizara ya Elimu imeipitisha Kamati kwenye mabadiliko hayo na muda siyo mrefu hata Bunge litapata fursa ya kuweza kupitishwa kwenye mabadiliko hayo, na kwa taarifa tu ni kwamba maboresho yaliyofanyika ni makubwa yenye tija kubwa kwa nchi yetu, tusubiri muda ufike tuyapitishe ili tuweze kunufaika na mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Salome Makamba unaipokea Taarifa hiyo?

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, taarifa hiyo siipokei, habari ya kusema hivi karibuni, Bungeni humu taarifa bado haijaingia kwa hiyo ninavyozungumza hivi sasa

ni kwamba Bunge halijapitisha mtaala mpya wa Serikali unaohusiana na elimu, bado hatujapitisha hilo ni moja.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, tumejadili hapa kuhusiana na namna ya kutengeneza mazingira rafiki ya uwekezaji, tulipitisha habari ya *blueprint economy,* kwamba tuwe na *one stop center* kwa ajili ya kumsaidia Mwekezaji anapokuja Tanzania asihangaike kukimbia huku na kule, lilikuwa Azimio la Bunge Serikali mpaka leo hakuna yaliyotekelezwa.

Mheshimiwa Spika, tulipitisha kuhusiana na mabadiliko ya Sheria ya Habari ili tupate uhuru wa Vyombo vya Habari, sheria imeletwa vipande vipande, zote za Habari bado zinamapungufu jambo ambalo linatutia doa! Mmesema tuwaoneshe watu mlango wa kupitia hiyo ndiyo milango sasa nawaonyesha. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Fedha……

**SPIKA:** Mheshimiwa Salome, sasa wewe unaweza kuwa ndiyo Mbunge wa kwanza kwenye uchangiaji huu kuambiwa muda wako umekwisha kengele imeshagonga. Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma atafuatiwa na Mheshimiwa Festo Sanga. Mtoa hoja ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kutoa shukrani na pongezi kwa Mheshimiwa Rais.

Kwanza naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Chiwelesa, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais pia tunamshukuru Mungu kwa kutupa Rais msikivu, kutokana na kipindi ambacho kwa kweli Mheshimiwa Rais amepokea madaraka haya hakupokea kwa njia ya kawaida, kwa hiyo hakukuwa na maandalizi. Nimshukuru pia kwa kuwa msikivu, tumepita

kwenye majungu mengi kuna watu wameitwa *Sukuma Gang* humu, kuna watu wameitwa majina tofauti, kuna watu wamepewa makundi tofauti, lakini tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa usikivu wake, ameendelea kuchapa kazi na kuwaacha wapuuzi wanaounda makundi na kuchafua wenzao waendelee nao, pia kazi zetu za Serikali ziweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana mimi ni mmoja wa watu ambao nilimwangalia sana Mheshimiwa Rais siku anaenda kwenye mkutano wa CHADEMA kule Kilimanjaro, yaani nilikuwa najiuliza hii CCM yetu tunakwenda kuitumbukiza wapi? Lakini baadae nikaja kuona mtu mpaka kufika kwenye cheo cha Rais ujue amepitia mambo mengi sana.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wengi Wana-CCM kule vijijini hawakumwelewa Rais, lakini baadae mimi nilivyokuja kutafakari, leo nataka niwaambie hivyo ndiyo maisha ya wanasiasa tunaishi, kwamba Mheshimiwa Rais alivyoenda kuwasikiliza na kuzungumza nao na kula nao chakula, haya ndiyo maisha yetu wanasiasa. Hata Watanzania mkituona tunazodoana humu na upinzani, tunatoka pale nje tunanunuliana chai.

Kwa hiyo, niwaombe Watanzania sikilizeni hoja za maendeleo kuliko kusikiliza mipasho ya kwenye majukwaa na Mheshimiwa Rais ameonesha mfano, ameenda kuwasikiliza wamepiga *cheers* lakini sisi huku tunapiga kazi. Kwa hiyo, haya ndiyo Maisha yetu wanasiasa huwa tunaishi hivi. Msije mkasikiliza maneno yetu huku juu wanasiasa halafu mkaenda kuandamana na kuumizwa miguu. Sikilizeni hoja zinazojibu matatizo ya wananchi wetu huko vijijini.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nazungumza suala la Mkaguzi *(CAG);* kwa kweli mimi ni Mbunge huu mwaka tunaenda wa

nane, nimemuona Mheshimiwa Rais juzi alivyozungumza kwa ukali mpaka akatumia na kaneno ka kizungu wale wenzangu kule hawakukaelewa akasema *stupid!* Ni kaneno kagumu sana sidhani kama anavyosikiliza Wabunge mnavyosema wale waone milango hakuna mtu anaweza kutoka kwenye mafuta kwa njia ya hiari nchi hii hayupo.

Mheshimiwa Spika, natoa mfano, Mheshimiwa Mbunge Ng'wasi Kamani kwenye Bunge lililopita yeye ni Mjumbe wa Kamati ya *LAAC,* alitoa mfano mzuri hapa akasema, kuna Mkurugenzi ametoka Ilemela ana tuhuma ya wizi wa shilingi bilioni 11 ameletwa kwa Mheshimiwa Musukuma, kwa miaka 22 sijawahi kupata hati chafu, nimo kwenye milioni sita, kwamba mtu anaiba huku halafu ninyi wenyewe mnamhamisha mnampeleka Halmashauri nyingine, huku anaendelea na uchunguzi anachukua pesa zetu kugharamia kesi ya Ilemela.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikuombe sana ngoma hii ikija humu kama alivyosema mwenzangu Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao hapa, katika vitu ambavyo Spika Mheshimiwa Dkt. Tulia tutakavyokukumbuka, hatutaki tena kupiga swaga, maana hizi swaga tumepiga mno kila taarifa ya *CAG* tunaongea, Serikali mnatutengenezea uadui bora mmalize wenyewe, tunataja watu watu hawachukuliwi hatua.

Mheshimiwa Spika, mtu anachukua kesi anaenda anapaki TAKUKURU, hivi TAKUKURU unachunguza mtu *CAG* ya mwaka jana halafu tena unakutwa na *CAG* ya mwaka huu? Jamani kama huko TAKUKURU na kwenyewe kuna TAKUKURU si na kwenyewe kuundiwe timu ya kuwachunguza? Tunaelekea wapi? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, haiwezekani tumejadili mambo haya mwaka jana tukataja watu, Kamati ya *LAAC* imeletwa taarifa na ikataja Halmashauri zaidi ya tisa, halafu hawahawa

wamepata Hati Chafu! Mheshimiwa Rais amefika hatua ya kusema pumbavu, sasa labda aje asomewe taarifa ya mwakani akiwa na kiboko mkononi, kama Bunge hatutachukua hatua ya kumsaidia! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama sheria zetu tulizitengeneza ni mbovu, hili Bunge ndiyo Bunge la wananchi wote, hatuwezi kuwa tunamuona Rais, ina maana kama Rais mwaka jana alisema atakayechezea pesa zangu za miradi ataitambua sura yangu halisi, maana yake hawa waliochezea hizi pesa wamemvizia Mama wakachungulia dirishani wakaiona sura? Sasa wamerudi kwa utaratibu mwingine haiwezekani! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kauli ya Mheshimiwa Rais mwaka jana mnisikilize vizuri, alisema jamani kama mnakula kuleni kwa urefu wa Kamba, hawa watu hawanunui kamba za katani, wananunua manati likijaa linatanuka! Lazima hili Bunge kwa mara ya kwanza tuoneshe mfano, haiwezekani. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana, naunga mkono hoja tunasubiri ngoma ije hapa tulale nao mbele *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Festo Sanga Mtoa Hoja ajiandae.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye hoja hii ya kumpongeza Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa *Engineer* Chiwelesa kwa kuleta hoja hii, mimi Mbunge wa Jimbo la Makete nina kila sababu za kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, kuna hoja kadha wa

kadha ambazo unaweza ukamzungumzia Mheshimiwa Rais kwa yale ambayo ameyafanya mengi.

Mheshimiwa Spika, kwanza ukiangalia kwenye sekta kwa mfano ya utalii, wakati dunia ina-*suffocate* kutokana na suala la *Covid* na watalii kupungua, Tanzania tumeweza ku-*excel* kwa kuongeza idadi ya watalii wengi kutokana na juhudi za Mheshimiwa Rais programu ya *Royal Tour*.

Mheshimiwa Spika, kwa idadi ya watalii tu, tumetoka kutoka 900,000 tumeenda 1,500,000 kwa kipindi hiki cha mwaka 2021 kuja mwaka huu. Haya yote ni matunda ya Mheshimiwa Rais. Ukienda kwenye suala la makusanyo ya fedha kwenye utalii, tumetoka dola milioni 1,300,000, tumeenda dola 2,500,000 ndani ya muda mfupi sana ambao Mheshimiwa Rais amefanya. Kwa hiyo, mimi kama Wabunge wengine, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi ambazo amezifanya.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwenye suala la miradi ya maendeleo, kuna miradi mikubwa ambayo tunaendelea nayo kama *SGR,* ununuzi wa ndege na ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere. Ni miradi ambayo *certificate* zina-*mature* mara kwa mara na zinatakiwa zilipwe. Hata hivyo, *at the same time* ukienda kwenye Halmashauri, miradi mingi inaendelea na fedha zinashuka kwa kiwango ambacho wakati mwingine ule haijawahi kushuka. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais anafanya kazi ngumu, anafanya kazi nzuri, anastahili sana kupongezwa.

Mheshimiwa Spika, nawaomba Watanzania ambao wanatufuatilia, wafahamu kabisa kwamba Mheshimiwa Rais anachohitaji sasa ni kutiwa moyo tu. Haya mambo anayoyafanya, ukienda kwenye Halmashauri, Wakurugenzi, miradi ilivyokuwa ni mingi, madarasa yanavyojengwa, kwenye Mataifa mengine tunaona wanavyolia. Nenda

kwenye suala la *inflation rate* kwa maana ya mfumuko wa bei, Taifa letu na Mataifa mengine yote yaliyoko kwenye Afrika Mashariki, Tanzania inafanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii yote ni kwa sababu Mheshimiwa Rais ameweza ku-*maintain* uchumi wa Taifa letu kwa kiwango kikubwa sana. Kilo moja leo hapa Tanzania, ndiyo, ni kweli vitu vimepanda bei, lakini la kujiuliza, na sehemu nyingine zipo kama Mataifa ya jirani yanayoendelea huko, sisi tuko chini sana kwenye suala la mfumuko wa bei. Pia bado Mheshimiwa Rais anatoa ruzuku kwenye mafuta, anatoa ruzuku kwenye mbolea, lakini bado wanafunzi wa vyuo vikuu anahangaika aweze kuwaongezea mikopo. Hii yote ni kwamba Mheshimiwa Samia anafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kazi nzuri ambazo anafanya Mheshimiwa Rais ikiwemo pia maridhiano haya ya kisiasa, na hata sasa ukiangalia anaendelea kuunda timu kwa ajili ya kuboresha diplomasia ya uchumi kwenye Wizara ya Mambo ya Nje, ameunda kikosi kazi chini ya Balozi Yahya Simba ili waangalie tathmini ya utendaji kazi wa Wizara ya Mambo ya Nje ili kuendelea kuboresha diplomasia yetu ya uchumi kupitia Wizara ya Mambo ya Nje. Ni jitihada za kweli za Mheshimiwa Rais anaendelea kuhakikisha Taifa letu linazidi kufunguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kwa haya anayoyafanya, maridhiano ya vyama vya siasa kwenye Taifa letu na demokrasia, hata vyama vingine viweze kuiga ambacho Mheshimiwa Rais anafanya. Mheshimiwa Rais anatengeneza maridhiano. Hata wao kwenye vyama vyao, tuwaombe wawe na maridhiano kwa sababu Taifa hili tumeamua kusamehe yote yaliyopita, tumeamua kuanza ukurasa upya. Hata wao wawe na ukurasa mpya kwa sababu kama wameridhia kuchukua ruzuku kutoka Serikalini kutokana na

idadi ya Wabunge na idadi ya kura, basi waridhie hata kuwasamehe hawa ndugu zetu ambao pia walikuwa na changamoto hizo. Kwa sababu ruzuku hiyo imetokana na wao wanayoichukua. Sasa huwezi ukatambua ruzuku, lakini usiwatambue Wabunge ambao tuko nao humu ndani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba tu, hata maridhiano hayo yaendelee kufanyika kwenye maeneo mengine. Jitihada za Mheshimiwa Rais ziguse kila mtu, na wao kwenye vyama vyao viweze kuwagusa.

Mheshimiwa Spika, mimi sina mambo mengi sana, lakini kwa niaba ya wananchi wa Makete, kwa kweli miradi ya maendeleo tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimuite Mheshimiwa Mhandisi Ezra Chiwelesa aje ahitimishe hoja yake.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kukushukuru na kushukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliopata nafasi ya kuchangia. Wamechangia takribani Waheshimiwa Wabunge 16 na michango yao karibu yote ilijikita kwenye yale maazimio yetu matatu ambayo niliyasoma hapa mwishoni. Kwa hiyo, nawashukuru sana kwa michango ambayo mmeitoa ya kumpongeza Mheshimiwa Rais katika maazimio haya matatu ambayo nimeyasoma hapa, ni michango mikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nadhani Watanzania ambao tunawawakilisha katika Bunge hili, sisi kama Wawakilishi wao ni mashahidi. Haya ambayo Waheshimiwa Wabunge

wameyasema ni dhahiri Mheshimiwa Rais anayaishi na wao wanayaona kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, labda nigusie tu kidogo kwa wale waliochangia katika habari ya kudumisha demokrasia. Nadhani karibu wote wameogelea hii nyanja ya demokrasia na wote ni mashahidi tunaona, shughuli za siasa zimeanza na zinaendelea. Hali kadhalika vile vikosi vya maridhiano ambavyo vinaendelea na kazi, vyote vinaenda vizuri. Kwa hiyo, tumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa hiki alichokianzisha. Maana kama wasingempa ushirikiano wale watu, tusingekuwa tumefika hapa.

Mheshimiwa Spika, pia ipo habari ya kukuza diplomasia ya kiuchumi. Hili jambo ni nyeti sana, wote tumesikia jinsi Waheshimiwa Wabunge wamechangia. Kuvutia wawekezaji kama Wabunge walivyosema, kama mazingira kwako siyo mazuri; na pia unapotafuta wawekezaji kwenye biashara, unaponyanyuka kuna baadhi ya watu utakutana nao unapata *confidence* ya kuja huku, kwa sababu mataifa mengi ya Afrika hayajulikani. Kwa hiyo, kazi kubwa anayoifanya Mheshimiwa Rais ya kuzunguka huku na huku, ndiyo tunaona matunda kama haya.

Mheshimiwa Spika, wote ni mashahidi, mwaka jana 2022 kwenye *Dubai Expo* mikataba iliyosainiwa pale mbele yake ilikuwa ni mingi na mizunguko yote ambayo amekuwa akiifanya tumekuwa tunaendelea kupokea neema kama hizo, na kama tulivyosema kwenye maelezo, hata ujio wa Makamu wa Rais wa Marekani pia umetufungulia fursa nyingine kwa vipengele ambavyo nimevitaja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pia hiyo ni sehemu na ni juhudi kubwa sana za Mheshimiwa Rais ambazo amezifanya, lakini kwenye sehemu ya tatu au sehemu C ambayo niliisema, kulikuwa na habari ya kumuunga mkono

Mheshimiwa Rais. Sasa nadhani wale wote ambao wameongelea Ripoti ya *CAG*, wote ambao wameongelea yale mambo yanayoendelea hapa sasa, hatumuungi mkono tu atekeleze, ni pamoja na kumlinda. Sasa kazi kubwa ambayo anayoifanya Mheshimiwa Rais kama haitapata *protection* ya Bunge kama ambavyo mmesikia Wabunge wanaongea, kesho na keshokutwa inaweza isionekane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nawashukuru Wabunge wote ambao wamechangia wakipaza sauti zao kwamba sasa kupitia Bunge hili tupate nafasi ya kuyalinda mazuri yote haya ambayo anayafanya Mheshimiwa Rais. Mazuri haya tutaweza kuyalinda kwa kuhakikisha kwamba yale yote ambayo yanapitishwa ndani ya Bunge yanasimamiwa na yanatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa dhahiri kabisa amesema yeye mwenyewe kwamba hata Bajeti ya *CAG* imeongezeka na bajeti ya ukaguzi wa ndani imeongezeka. Sasa kazi kubwa ambayo anaifanya Mheshimiwa Rais, Bunge tunapopitisha bajeti ambayo imeongezeka kama hivyo, maana yake inampa *freedom CAG* na wakaguzi wa ndani kuweza kufanya ukaguzi mzuri wa hizi fedha ambazo tunazipitisha kwa niaba ya Watanzania na fedha ambazo Mheshimiwa Rais anazihangaikia usiku na mchana ziweze kuja kuwasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kumalizia, niwashukuru Wabunge wote ambao wamechangia, ninaamini mengine sasa yanabaki mezani kwako kwa ajili ya utekelezaji kwa sababu ni Maazimio ya Bunge. Yale yote ambayo yameombwa na baadhi ya Wabunge nadhani umeyasikia, muda ukiwadia, kwa sababu Ripoti ya *CAG* bado haijaja humu, ndiyo maana sikuiongelea katika azimio hili.

Itakapofika, ikishapokelewa ikawa mali ya umma ikapita ndani ya Bunge, nadhani Kiongozi wetu wa Mhimili atajua jinsi gani ataenda nayo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema haya, naomba kutoa hoja.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Ezra Chiwalesa. Sasa nitawahoji Wabunge ambao wanaafikiana na Azimio la Bunge la Kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuimarisha demokrasia nchini na kukuza diplomasia ya uchumi. *(Makofi)*

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Bunge la Kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuimarisha demokrasia nchini na kukuza diplomasia ya uchumi liliridhiwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mhandisi Ezra Chiwelesa kwa azimio hili ambalo amelileta la kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhusu kazi nzuri anayoifanya. Anafanya kazi nzuri kwenye nyanja nyingi, lakini yeye amechagua katika haya maeneo ya diplomasia ya uchumi na pia demokrasia nchini. Kwa hiyo nakupongeza sana Mheshimiwa Ezra kwa kuyaona mambo haya mazuri. *(Makofi)*

Pia niwapongeze Waheshimiwa Wabunge, kila mmoja wenu ameshiriki katika mjadala huu kikamilifu na kila mmoja ameeleza namna yeye anavyoona mawanda yalivyo mapana katika maeneo haya mawili. Kwa hiyo, na ninyi nyote nawapongeza sana. *(Makofi)*

Kwa muktadha huo, nami niungane nanyi kumpongeza sana Mheshimiwa Rais katika maeneo haya ambayo anafanya kazi nzuri sana kwenye hili eneo la diplomasia ya uchumi, sina haja ya kurejea lakini mmetoa mifano mingi sana. Naamini kwa sababu tutaendelea kujadili taarifa za Wizara mbalimbali na tutazisikiliza Kamati zetu zinasemaje katika hayo mengi yatakayoendelea kujitokeza na tutaendelea kuona kwa kiasi gani Mheshimiwa Rais ametimiza ahadi alizokuwa amewapa wananchi mwaka jana 2022 kwenye bajeti. *(Makofi)*

Wakati huo huo tutapata fursa ya kuendelea kushauri Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Rais katika kuboresha hapa na pale ili mambo yaendelee kuwa mazuri. Sasa pongezi kama hizi ni za muhimu sana hasa kwa Mhimili kama wa Bunge kwa kuwa Rais anapofanya vizuri, kwa sababu ni kazi yetu sisi kuishauri na kuisimamia Serikali, anapofanya vizuri ni muhimu sana tumtie moyo.

Kwa hiyo, ni kazi ambayo kwa kweli itakuwa endelevu. Hatufanyi kila siku, lakini sasa Wabunge wanayo nafasi, watampongeza hapa na pale, lakini inapotokea jambo kama hili, Bunge kwa pamoja sote tumekusudia kumuunga mkono Mheshimiwa Rais, lakini pia kumtia moyo kwa kazi nzuri anayoifanya kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, azimio hili la Bunge limepita rasmi. Bunge leo limempongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuimarisha

Diplomasia ya Kiuchumi na pia kwa kuendeleza demokrasia nchini Tanzania. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna mambo mawili madogo; ambo la kwanza ni hii Taarifa ya *CAG* ambayo imepokelewa mwezi uliopita na Mheshimiwa Rais, ambapo kwa utaratibu wa sheria zetu na Katiba yetu, ile taarifa italetwa hapa Bungeni. Kwa sheria ile ambayo tumetunga sisi na kwa mujibu wa Katiba yetu, ile taarifa itakapoletwa hapa Bungeni ndiyo inakuwa wazi kwa umma. Kwa hiyo, ile taarifa haiko wazi kwa umma mpaka sasa. *(Makofi)*

Sasa kwa nini nalazimika kusema haya? Ni kwa sababu hata sisi katika michango yetu leo, na kwa sababu leo ndiyo tumeanza tunaelekea huko mbele na watu wangependa sana kuzungumzia taarifa hii; ni kweli hautazuiwa kuzungumzia kwa maana ya pengine kutolea mfano kwamba umesoma kifungu hiki, kifungu kile; lakini kwa maana ya taarifa hii, namna ya kufanyiwa kazi na Tanzania, nasi ndiyo tunafanya kazi kwa niaba hiyo, lazima ikishafika hapa Bungeni ipelekwe kwenye Kamati zetu za usimamizi. Ikishaenda kule, wale wanapata nafasi ya kupitia zile taarifa kwa kirefu na kwa undani na kuwasikiliza wale ambao zile taarifa zinahusu maeneo yao. Wakishamaliza ile kazi wanaleta hapa ndani. Wakileta hapa ndani, ndiyo mjadala unaanza rasmi wa Bunge kujadili Taarifa ya *CAG*.

Baada ya huo mjadala, tunaazimia sasa kama Bunge tunaiambia Serikali nini? Kwa hiyo, huo ndiyo mchakato wa namna Ripoti ya *CAG* inavyofanyiwa kazi. Haijalishi ni mambo mazito kiasi gani yaliyotajwa mle ndani, lakini utaratibu tuliojiwekea lazima ufuatwe. Kwa nini ni lazima? Kwa sababu *CAG* ni jicho la Bunge. Yeye *CAG* siyo Bunge, hafanyi maamuzi kwa niaba ya Bunge. Bunge linafanya maamuzi lenyewe. Ili Bunge liweze kufanya maamuzi lenyewe, lazima tufuate ule utaratibu wa Kamati kushughulika kwanza na

hayo mambo kutuletea hapa ndani ndiyo tunafanya maamuzi. Nadhani nimeeleweka.

Kwa hiyo, yeyote aliyetajwa na *CAG*, sijui ambaye hakutajwa, ambaye hajafanya nini, sisi ndio waamuzi wa mwisho kwenye jambo hili. Kwa nini? Kwa sababu tutakuwa tumeshamsikiliza, na sisi tumejiridhisha kwamba hiki kiko hivi, kiko hivi, kwa hiyo tunaamua hivi. Ndiyo maana huwa tunafanya maazimio baada ya huo utaratibu kukamilika.

Ndicho ambacho mwaka jana 2022 mwezi wa Kumi na Moja tulikifanya. Tulitumia hapa wiki nzima kujadili taarifa ya *CAG* ya Mwaka 2020/2021. Tulipomaliza ule mjadala, kama ambavyo mwaka huu tumepewa hii, mwaka jana tulipewa nyingine ndiyo tukaijadili mwezi wa Kumi na Moja, tukaazimia mambo kadhaa.

Nakumbuka wakati nikipeleka sasa Serikalini hayo maazimio yenu Wabunge, ama maazimio ya Bunge, niliiambia Serikali haya ndiyo Maazimio ya ya Bunge pamoja na mengine aliyoyasema *CAG*. Nilisema hivyo, na niliwakumbusha kwamba, Waheshimiwa Wabunge, taarifa za Bunge hili la bajeti, Serikali inapokuja mbele yenu, yatazameni haya pia utekelezaji wa maeneo ambayo *CAG* aliyasema ambayo yako kwenye sekta zenu mnazozisimamia. *(Makofi)*

Sasa Kamati mmemaliza ukaguzi wa miradi, Kamati mmemaliza kazi ya kuisikiliza Serikali, kwa maana ya bajeti zitakazoingia humu ndani; kama hilo hamkulifanya, ni la kwenu. Hapo msiseme Spika hakuwapa nafasi. Nafasi mliipata ndefu kabisa mwezi wa Kumi na Moja, na mwaka huu hapa katika Bunge hili mmepewa wiki tatu za kukaa kwa ajili ya kazi hiyo. Kama hamkuifanya mpaka leo, ni la kwenu na ni letu Bunge zima. Ndiyo utaratibu wa taarifa. Siyo kwamba tunasikiliza jambo fulani halafu tunataka kwenda nalo kwa sura fulani hivi, hapana. Lazima utaratibu ufuatwe

na kama hatukufanya, basi tuendelee kujifunza na tuendelee kujirekebisha Bunge lifanye kazi yake linaposikia kuna mahali hapako sawasawa. Liisimamie Serikali, liishauri Serikali. Sasa watu watasema Mheshimiwa Spika anasema hivi, lakini Mheshimiwa Rais yeye hakumwona. Nilimwona, nami nilikuwepo.

Pale kuna mambo mawili ambayo yalizungumzwa pale, wale waliofuatilia na wale ambao tulikuwepo nadhani tuliona. Mheshimiwa Rais aliipokea Taarifa ya *CAG* na akaagiza Serikali ije kujibu Bungeni. Alisema hivyo kwa sababu anafahamu Katiba inasemaje na sheria inasemaje. Ndiyo maagizo aliyotoa kuhusu Taarifa ya *CAG;* kwamba yale aliyosema watu watupishe, kuna jambo la pili alilolizungumza pale ambalo pia linazungumzwa, lakini watu wanalichanganya na Taarifa ya *CAG*. Lile haliko kwenye taarifa ya *CAG,* halijafanyiwa ukaguzi, ni Serikali yenyewe imeliona hilo. Mheshimiwa Rais yeye mwenyewe ameliona hilo la madai ya kuongezeka kwa kiasi kikubwa cha fedha kwenye malipo ya ndege ya mizigo. *(Makofi)*

Sasa haya kwa sababu yalisemwa siku ambayo Mheshimiwa Rais alikuwa anapewa taarifa, watu wameyaweka yote pamoja, wanaona kama Rais alishafanya pale maamuzi. Nimeona mijadala sehemu nyingine, wanaona kama Rais alivyopokea ile taarifa, basi ndiyo ametoa maelekezo. Hapana. Maelekezo pale yalikuwa mawili tofauti. Walioelekezwa kwa sura ile ni wale walioongeza fedha ambayo haina uhusiano na Taarifa ya *CAG*.

Taarifa ya *CAG* aliiagiza Serikali kwamba Waheshimiwa Mawaziri na Wataalamu wenu kwenye Wizara zenu mnapoenda huko Bungeni katoeni majibu kuhusu hoja ambazo *CAG* amezieleza. Nadhani hilo limeeleweka. Kwa hiyo lina sura hiyo. Sasa watu wasichanganye hayo yote

mawili wakaona yote yako kwenye Taarifa ya *CAG*. Yale yaliyo kwenye Taarifa ya *CAG* utaratibu ni huo nilioueleza ambapo sheria tumeitunga sisi wenyewe, lazima ifanyiwe kazi wale watu wasikilizwe halafu ndiyo iletwe hapa ndani tuanze kuazimia. Kwa hiyo, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo utaratibu.

Sasa jambo la pili na la mwisho ni kuhusu vyombo vya habari. Nilishawahi kuzungumza huko nyuma, nirejee tena kwa sababu ndiyo tunaanza Bunge leo na tutakuwa hapa kwa kipindi kirefu tukishirikiana.

Niwaombe tena habari za upotoshaji kuhusu Bunge hazipendezi hata kidogo. Kwa nini? Kwa sababu Bunge lipo wazi, ni la wananchi na lipo kwa ajili yenu pia waandishi kwa sababu ninyi ndio mnaowajulisha wananchi yanayoendelea hapa ndani. Kwa hiyo, haipendezi kupeleka taarifa za upotoshaji kwa wananchi. Mnaibua hisia ambazo hazina maana yoyote. Gazeti la Mwananchi, *Jamii forum* tunawategemea sana kuwapelekea wananchi taarifa sahihi. Tusipeleke kwa wananchi taarifa za upotoshaji. Haipendezi hasa pale ambapo hamjaomba taarifa na wala hamjanyimwa.

Kwa hiyo, kama kuna jambo halieleweki uliza kwanza ili chombo chako cha Habari, ninyi ndiyo mnaosema watu wasikilizwe. Kwa hiyo, na sisi mtusikilize kwanza ili uelewe vizuri kabla hujatoa hiyo taarifa yako.

Kwa hiyo, taasisi ama Mhimili wa Bunge unawakumbusha Waandishi wa Habari kufanya kazi yao kwa weledi. Milango yetu iko wazi na itaendelea kuwa wazi kwa ajili ya kutoa ufafanuzi pale ambapo linajitokeza jambo lolote. Tusingependa sisi kama mhimili ambao ni Wawakilishi wa Wananchi, taarifa ziwe zinapelekwa huko zinazozua taharuki. Haipendezi.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye ni Mwenyekiti pia wa Kamati ya Wabunge wa CCM, anawatangazia Wabunge wa CCM kwamba kikao kitaanza saa 9.00 alasiri mahali ambapo mmejulishwa kwamba kikao hiko kitafanyika. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nawashukuru tena kwa ushirikiano. Sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 7.00 mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 5 Aprili, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*